Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

"Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wale wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu" (2:184)

JUZU 77 No. 194 | JUM II - RAJAB 1439 AH | MEI 2018 | AMMAN 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Nyota za Kufuata: Hamza Ibn Abdul-Muttalib (r.a.)

Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah,Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba)alisema:

"Hadhrat Masihi Mauud a.s. alisema ya kwamba: "Wakati wa ujio wa Mtume Mtukufu s.a.w. taifa la Kiarabu kutokana na khulka, utamaduni na hali yake ya kiroho lilikuwa na hali ya namna gani? Katika kila mahala hali ya kivita, kunywa pombe, uzinzi, ujambazi ilmuradi kila aina ya uovu ulikuwa ukipatikana. Kulikuwa hakuna mahusiano yoyote kwa Mwenyezi Mungu na kwa khulka njema, kila mmoja wao alikuwa akijifanya kuwa firauni lakini kutokana na ujio wa Mtume Mtukufu s.a.w. walipoingia katika Uislamu basi mapenzi ya Mungu na umoja wa namna fulani yalizalika nafsini mwao ya kuwa kila mmoja wao akawa tayari kufa katika njia ya Allah nao wakadhihirisha uhakika wa kufanya baiati na kwa matendo yao wakaonesha mfano wake.



Sehemu ya waumini ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London ambao Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Huzur anasema ya kwamba, "Masahaba (r.a) wa Mtume Mtukufu s.a.w walionesha mfano wa namna gani wa uaminifu wao ambao mfano wake ulikuwa haupatikani kabla wala hautapatikana hapo mbele lakini Mwenyezi Mungu Anaweza kufanya Amtakaye na mifano hii inawanufaisha wengine na katika Jumuiya hii Mwenyezi Mungu Anaweza kuonesha mifano ya namna hii.

Huzur anasema ya kuwa, "Mwenyezi Mungu katika kuwasifia masahaba r.a Alisema ya kwamba:

Wapo watu miongoni mwa waaminio waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Allah: hivyo baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea, wala hawakubadilika hata kidogo. (33:24)."

Aya zinazowasifia masahaba kama zikusanywe basi aya hii ni mfano uliotukuka. Basi mifano hii ya kujitolea na ya wema ni mifano ya kuigwa

Endelea uk 2

Ramadhan: Mwezi wa Funga

• Je, Swaumu ni kuachana na kula tu?

Maktaba Yetu

Kufunga ni ibada inayopatikana katika dini zote za ulimwengu kwa sura moja au nyingine. Qur'ani Tukufu inasema:

"Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wale wa kabla yenu ili mpate kumcha Allah"



Katika Uhindu, kufunga hujulikana kama 'varat' au 'barat'. *Wajinyimao* tu ndio wanaotakiwa kujiepusha na kula kwa siku arobaini. Kwa waumini wengine, mchakato wa kufunga ni rahisi zaidi; wanaruhusiwa kula matunda, kunywa maziwa na maji kwa uhuru na vyakula tu ambavyo vinapikwa kwa moto haviruhusiwi wakati wa kufunga. Maelezo haya na zaidi juu ya kufunga katika Uhindu yanaweza kupatikana katika *Sanatan Dharm*. Katika Ukonfyushasi, waumini wanaofunga wanatakiwa kuvaa nguo safi za kitani na kubadilisha vyakula vyao. Kwa Wabuddha, watawa wa kike na wa kiume wanapata mlo mchana tu na kutokula tena. Sababu kuu za kufunga ni za kiafya na kuwezesha kutaamali kwa murua. Mbali na watawa, Wabuddha hawana saumu kabisa, kwa sababu wanaamini kuwa inatofautiana na 'Njia ya Kati'. Katika Uyahudi, kabla ya Uhamisho wa Babilonia, kufunga kulifahamika kama '*kutesa nafsi*'. Katika Mambo ya Walawi 23:27 tunayo, "Siku ya kumi ya mwezi wa saba kutakuwa na siku ya upatanisho, itakuwa ni kusanyiko takatifu; nanyi mtatesa nafsi zenu. "Hii ni funga ya mwishoni mwa mwaka ambayo huangukia siku ambayo Mungu Aliwapa wafuasi wa Musa (as) kutoka kwa Farao. Wakati wa Uhamisho wa Babilonia, funga nne zaidi ziliwekwa kuadhimisha uvamizi na

Endelea uk 4

Hawapati Usingizi!

Na Mohammed Kazema

Miongoni mwa aya inayowanyima usingizi, inawapa hofu na huzuni maadui wa neema za Allah kwa wanadamu ni aya hii:-

يٰبَنِيْٓ اٰدَمَ اِمَّا يَاْتِيَنَّكُمْ رُسُلٌ مِّنْكُمْ يَقُصُّوْنَ عَلَيْكُمْ اٰيٰتِيْ ۙ فَمَنِ اتَّقٰى وَاَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ۝

[Al-A'raf :36]

Yaani:- Enyi wanadamu bila shaka watakujieni (watakufikieni) mitume kutokana nanyi watakusomeeni aya zangu basi yule ataye ogopa na kufanya wema haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

Kama jinsi hiyo aya isemavyo, kwamba mitume watafika kutoka miongoni mwetu sisi wanadamu na kazi yao itakuwa kufundisha aya za Allah kwa sababu toka azali ni asili ya mwanadamu "kusahau" mafundisho kwani si tunaona mtu anaweza kuambiwa jambo fulani lakini baada ya saa kadhaa kupita anakuwa kisha sahau alichoambiwa sembuse takriban miaka 1400 Qur'an ilipoteremka??!!, Je binadamu au Waislamu bado wanakumbuka na kujua mafundisho yake?. Vipi hali za wasio Waislamu leo?, hawa wote lazima wafundishwe Qur'an sheria ya mwisho.

Kulingana na hiyo aya , mlango wa kuja Mtume ndani ya Uislamu upo wazi.

Kwa yule anayetafuta ukweli basi ni ukweli upi autafutao nje ya Qur'an?. Naam kuna ukweli nje ya Qur'an lakini kama utapingana na Qur'an yaliyo maneno ya Allah je, unaweza kukubali maneno ya mwanadamu kirahisi?. Naam, kuna ukweli nje ya Qur'an lakini Qur'an ndiyo msingi wa kweli yote.

Hiyo aya iko wazi kabisa na kama fikra za mtafuta ukweli zitakuwa "huru" fikra zilizoachwa kwenye mikono ya Allah ili Azitawale kwani ni Yeye Aliyetupa hizo fikra na Anajua madhaifu ya fikra zetu, basi bila shaka Allah Aliye Mtukufu Atakuongoza.

Amin ya rabb al'alamin.

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KIUKENI KUTA HIZI

Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ina imani thabiti na katu isiyoyumba kwamba Khalifa anachaguliwa na Allah. Katika hili Waahmadiyya katu hawatazami nyuma. Waaminio wanapewa taadhima tu ya kufanya kazi hiyo ya kumchagua Khalifa lakini kimsingi hiyo ni kazi ya Muumbaji wa mbingu na ardhi.

Kwa mantiki hiyo basi Khalifa ana mawasiliano moja kwa moja na Allah. Maombi yake yanapokelewa sana. Hivyo sisi katika Jumuiyya ya Ahmadiyya hakuna kitu tunachokiheshimu na kukienzi kama kauli na maelekezo ya Khalifatul Masihi (atba). Hivyo karibuni Khalifatul Masihi – V (atba) katika moja ya hotuba zake za Ijumaa alituagiza kwa msisitizo mkubwa usomaji wa kitabu cha Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) 'Safina Ya Nuhu'. Tunakumbushana juu ya ulazima na umuhimu wa kufuata agizo hilo la kiongozi wetu mpendwa. Kwani kama tulivyosema hapo juu maelekezo ya Khalifa wa Mwenyezi Mungu yanakuwa yamepata baraka kubwa kutoka kwa Allah. Safina Ya Nuhu ni bahari ya maelezo na ufafanuzi wa Qur'an Tukufu. Ni kitabu ambacho kina kazi moja ya kusafisha nafsi. Na kwa sababu ni bahari pana tutajikita katika sehemu moja nayo inahusu 'nyumba'.

Kwa msaada wa Allah tumejaliwa kujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya na kwa kufanya hivyo tuko nje kusubiri kuingia nyumbani. Lakini kabla ya kuingia katika nyumba hiyo ambayo ni ya Masihi Aliyeahidiwa (as) yapo masharti na kanuni ambazo hivyo vyote unatakiwa uvitekeleze ili upatiwe ufunguo wa kuingia katika nyumba hiyo. Na hivyo tunakumbushana ambayo Masihi Aliyeahidiwa (as) ametueleza ya kwamba watakaoruhusiwa kuingia katika nyumba hiyo ni wale ambao watafuata kwa dhati na kwa vitendo mafundisho aliyopewa (Masihi Aliyeahidiwa) na Mwenyezi Mungu. Hivyo wanaoruhusiwa kuingia katika nyumba hii wanatakiwa wawe na imani thabiti ya kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kila kitu na wakati wa kuomba wawe na imani hii. Na bila ya imani hii hakuna atakayeruhusiwa kuingia katika nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa (as).

Anaendelea kututahadharisha Masihi Aliyeahidiwa ya kwamba yule ambaye anashikilia uongo na udanganyifu huyo asijidanganye kwamba atapewa nafasi ya kuingia katika nyumba hii. Asiyetanguliza dini, akatawaliwa na mapenzi ya dunia huyo naye hawezi kuingia katika nyumba hii. Na yeyote yule asiyeacha tendo baya kama kunywa pombe, kucheza kamari, kutazama wanawake, kuzini, hiyana na rushwa na akakosa kutubia huyo pia hana nafasi katika nyumba hii. Asiyedumu kusali sala tano kwa unyenyekevu atambue mlango wa nyumba hii umefungwa. Mtu asiyewaheshimu wazazi wake isipokuwa wakati wamemlazimisha kinyume cha Qur'an Tukufu hayumo katika nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa (as).

Kama tulivyosema, Safina Ya Nuhu ni bahari pana na inatakiwa kuogelea katika bahari hiyo kila siku. Tunakumbushana ya kwamba tuendelee kusoma kitabu hicho cha Safina Ya Nuhu ili kupata faida na hatimaye kupata shabaha ya msingi ya kuumbwa kwetu ambayo ni kumuabudu Allah.

Hamza ibn Abdul-Muttalib(r.a.)

Kutoka uk. 1

kwa ajili yetu.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema ya kwamba: "Nimeendelea kueleza hali za masahaba r.a. ambao baadhi yao walikuwa masahaba wa Badri yaani walioshiriki katika vita ya Badr na wengine pia lakini kisha wazo lilinijia ya kuwa kwanza nieleze hali za wale walioshiriki vita ya Badri, hao wana cheo makhsus na ni watu ambao Mwenyezi Mungu Aliwaridhia, hivyo leo nitaeleza kuhusu Hadhrat Hamza Bin Abdul Muttalib r.a, ambaye anajulikana kwa laqabu ya Sayyid ush Shuhadaa na pia kwa jina la Asadullah na Asad ur Rasuul.

Hadhrat Hamza r.a alikuwa mtoto wa Hadhrat Abdul Muttalib (kiongozi wa kabila la Quraish) na baba mdogo wa Mtume Mtukufu s.a.w. Mama yake alikuwa anaitwa Hala. Yeye alikuwa mkubwa katika umri miaka miwili au kutokana na riwaya nyingine miaka minne kuliko mtume s.a.w, naye pia alikuwa ndugu wa kunyonya ziwa moja na Mtume s.a.w. Kulikuwa na mtumwa mmoja aitwaye Thaubia aliyewanyonyesha wote wawili. Yeye alijaaliwa kusilimu katika mwaka wa sita wa utume.Tukio lake la kusilimu kama lilivyoelezwa na Hadhrat Musleh Mauud r.a. nitaeleza muhtasari wake.

Siku moja Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa ameketi kwenye jiwe moja lililopo kati ya milima ya Safa na Marwa akitafakari ni kwa namna gani Tauhidi ya Mwenyezi Mungu itastawishwa. Hapo akaja Abu Jahal na kumkaripia, "Ewe Muhammad unaendelea na mambo yako kama kawaida"; na pamoja na kusema hayo akaanza kumtukana Mtume saw, Mtume saw akaendelea kumsikiliza kwa utulivu na kumvumilia tu na hakunena hata neno moja. Abu Jahal alipomaliza kumtukana Mtume saw hapo akajisogeza mbele na kumchapa kibao Mtume saw; hata hivyo Mtume saw hakusema lolote. Mahala Mtume saw alipokuwa amekaa na Abu Jahal alikuwa akimtukana, mbele kidogo ilikuwa nyumba yake Hadhrat Hamza r.a, wakati ule Hadhrat Hamza r.a alikuwa bado hakusilimu na ilikuwa kawaida yake ya kuwa kila siku asubuhi akienda kuwinda kwa mishale na upinde wake na kurudi jioni na kukaa katika vikao vya Maquraishi. Siku ile Abu Jahal alipomtukana mtume s.a.w na kumtendea vibaya, Hadhrat Hamza alikuwa amekwenda kuwinda lakini kwa bahati kilichotokea ni kwamba Abu Jahal alipokuwa akifanya hivyo basi mtumishi mmoja wa Hadhrat Hamza alikuwa akitizama tukio hilo lote. Abu Jahal alipokuwa akimshambulia Mtume s.a.w kwa kumtusi matusi mengi kupita kiasi huku Mtume s.a.w kwa ukimya na utulivu akivumilia matusi yake, mtumishi huyo akiwa amesimama mlangoni aliendelea kushuhudia mandhari haya. Hadhrat Musleh Mauud r.a. anaandika ya kuwa, "Hakuna shaka ya kuwa yeye alikuwa mwanamke tu na alikuwa kafiri lakini katika zama zile watu wa Makka walipokuwa wakiwadhulumu watumwa wao wakati huo huo walikwepo watu wema waliokuwa wakiwatendea watumwa wao kwa wema na baada muda fulani wale watumwa walikuwa wakijulikana kuwa sehemu ya familia yao. Vivyo hivyo alikuwa mtumishi huyu wa Hadhrat Hamza r.a. Wakati yeye aliona mandhari haya yote kwa macho yake na kuyasikia kwa masikio yake basi akashikwa na hisia fulani lakini hakuwa na uwezo wa kufanya chochote, akaendelea kuyashuhudia na kuyasikiliza na hasira ikaendelea kumpanda ndani kwa ndani. Jioni Hadhrat Hamza r.a. aliporudi na kuingia nyumbani kwa maringo akiwa ameshika mishale na upinde mkononi mwake basi mtumwa huyu akasimama mbele yake naye alikuwa akificha hasira yake kwa muda mrefu akamwambia Hadhrat Hamza r.a. ya kuwa, "Wewe hujisikii haya, huku unajifanya kuwa jasiri mkubwa! Hamza kwa kuyasikiliza hayo akashikwa na mshangao na kumwuliza kuwa kilichotokea ni nini? Mtumishi huyu akamjibu kuwa kilichotokea ni hiki ya kwamba mpwa wako (Muhammad saw) alikuwa ameketi hapa na Abu Jahal akaja na kumshambulia na kumtukana sana na kumchapa lakini Muhammad s.a.w. hakutamka lolote mbele yake na akaendelea kuyasikiliza kwa utulivu.

Hadhrat Hamza r.a. kwa kulisikiliza tukio hilo alighadhabika sana, wakati huo huo akaelekea Kaaba na kufanya Tawwaaf kisha akaelekea mahala ambapo Abu Jahal alikuwa amekaa akizungumza na watu akiwasimulia tukio hilo kwa kibri ya kwamba leo alimtukana Muhammad na kumtendea vibaya.

Hadhrat Hamza r.a mara baada ya kufika pale akampiga Abu Jahal kwa upinde wake na kumwambia ya kuwa, "Wewe unawasimulia matukio ya ujasiri wako na kuwaambia kuwa ulimdhalilisha Muhammad sasa mimi nakudhalilisha ikiwa wewe una uwezo wa kujibu basi sema chochote? Abu Jahal wakati ule alikuwa anajulikana kama mfalme jasiri na alikuwa kiongozi wa watu. Watu wake walipoona mandhari haya basi wakainuka kwa hasira na jazba na kujaribu kumshambulia Hamza. Abu Jahal aliyekuwa ameshikwa na haiba akawazuia na kusema kuwa acheni tu kwani mimi nilikuwa nimekosea na Hamza anachokisema ni sahihi.

Hadhrat Hamza r.a. katika kikao kile kile alijitangaza kuwa mwislamu na kumwambia Abu Jahal ya kuwa, "Wewe ulimtukana Muhammad saw kwa sababu yeye anasema ya kuwa 'mimi ni mtume wa Mungu na Malaika huniteremkia', sikiliza kwa makini kuwa mimi pia kuanzia leo najiunga na dini yake na kusema kama asemavyo Muhammad s.a.w. ikiwa una uwezo basi njoo ushindane nami na kwa kusema hayo Hadhrat Hamza r.a akasilimu.

Imeelezwa katika riwaya mbali mbali kuwa baada ya kusilimu kwa Hadhrat Hamza r.a imani wa Waislamu wa Makka ilipata kuimarika zaidi. Hadhrat Hamza r.a pia alihamia Madina pamoja na Waislamu wengine, lakini hata baada ya kuhamia Madina makafiri waliendelea na mipango yao, hivyo Waislamu walilazimika kuwa makini na ili kwa lengo la kukabiliana na mipango ya makafiri katika mwaka wa pili wa Hijria mwezi wa Rabi ul Awwal Mtume Mtukufu s.a.w aliwatuma mahala fulani kikundi cha wahamiaji wapatao thelathini chini ya usimamizi wa Hadhrat Hamza r.a. Hadhrat Hamza r.a na wenzake walipofika maeneo yale basi wakamkuta kiongozi wa Makka Abu Jahal pamoja na wanajeshi mia tatu akiwa anawasubiri. Idadi ya Waislamu ilikuwa thelathini tu ilhali wapinzani walikuwa mia tatu. Wakaja ana kwa ana na kupanga mistari kwa ajili ya vita lakini kiongozi wa maeneo yale aitwaye Majdi Bin Amr aliyekuwa na mahusiano na pande zote mbili akapatanisha kati yao na vita haikutokea.

Baada ya kuhamia Madina pamoja na Waislamu wengine hali ya kiuchumi ya Hadhrat Hamza r.a pia iliporomoka. Siku moja Hadhrat Hamza r.a alimjia Mtume s.a.w na kumwambia ya kuwa apatiwe kazi fulani ili aweze kutafuta

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Hamza ibn Abdul-Muttalib(r.a.): Sayyid-ush-Shuhadaa

Kutoka uk. 2

njia za kujikimu. hapo Mtume saw akamwuliza ya kuwa, "Ewe Hamza je kuzingatia heshima ya nafsi ni bora zaidi au kuipoteza? Hadhrat Hamza r.a akamjibu ya kwamba, "mimi napenda kuizingatia heshima ya nafsi yangu"; hapo Mtume s.a.w. akasema basi ilinde heshima ya nafsi yako kisha akamsisitiza kuomba maombi mengi na kumfundisha baadhi ya maombi. hivyo imesimuliwa na Hadhrat Hamza r.a ya kwamba Mtume Mtukufu saw alisema ya kuwa uishike dua hii kwa nguvu zote isemayo kuwa, "Ewe Allah nakuomba kwa Jina lako na kwa ridhaa Yako." kisha kwa siku zote yeye alishuhudia matokeo ya maombi yake maishani mwake.

Mnamo mwaka wa pili wa Hijra vita ya Badri ilitokea, wakati wa vita vya Badri upande wa makafiri Aswad Bin Abdul Asad Makhzumi alijitokeza ambaye alikuwa mtu mbaya mwenye kutisha sana. Yeye alipanga nia ya kwamba lazima atakwenda kunywa maji kwenye kisima cha Mtume s.a.w. au atakibomoa au kukiharibu na kuchafua maji yake au atakufa karibu nacho. Yeye alijitokeza kwa nia hii, Hadhrat Hamza r.a. akatoka kukabiliana naye. Wakati wote wawili wakisimama ana kwa ana basi Hadhrat Hamza r.a kwa kumshambulia kwa upanga wake akakata mguu wake, yeye alikuwa karibu na bwawa lile. Yeye akaanguka chini na kuanza kujisogeza kwenye bwawa lile ili aweze kutimiza kiapo chake. Hadhrat Hamza r.a. akamfuata na kummaliza pale pale.

Katika vita vya Badri idadi ya makafiri ilikuwa kubwa sana kuliko idadi ya Waislamu, usiku kucha Mtume s.a.w aliendelea kumwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu mkubwa. Hadhrat Ali r.a anasimulia ya kwamba Utbah Bin Rabiya na nyuma yake mwanaye na nduguye pia walijitokeza na kusema kwa sauti ya juu ya kuwa ni nani atakayejitokeza ili kushindana nasi? Utbah alisema ya kuwa, "sisi tumetoka kwa lengo la kupigana na watoto wa baba yetu mdogo tu." Hapo Mtume s.a.w akasema Ewe Hamza, Ewe Ali, Ewe Ubaida Bin Haarith jitokezeni. Hamza r.a akamfuata Utbah. Hadhrat Ali r.a anasema ya kuwa, "mimi nikamlenga Sheba na Ubaida na Waliid wakapigana. Hadhrat Ali r.a na Hadhrat Hamza r.a wakawaua maadui zao. Hadhrat Hamza r.a alionesha ujasiri wake mkubwa katika vita vya Badri, Umayya Bin Khalf alisema ya kuwa mtu huyu ametuletea hasara kubwa sana.

Katika vita vya Uhud pia Hadhrat Hamza r.a alijaaliwa kupigana kwa ushujaa mkubwa sana, maelezo yake yamehifadhiwa katika kitabu cha Bukhari ambapo imesimuliwa na Umair Bin Ishaka ya kwamba, "Siku ya vita vya Uhud Hadhrat Hamza r.a alikuwa akipigana vita kwa kuzitumia panga mbili, alikuwa mbele ya Mtume s.a.w na alikuwa akisema ya kwamba, "mimi ni simba wa Mungu" mara alikuwa anajisogeza mbele na mara alikuwa akirudi nyuma, katika hali hiyo ghafla akateleza na kuanguka chini. Wahshi Aswad akamwona akianguka chini hapo akamshambulia kwa mkuki wake. Hadhrat Hamza alikufa shahidi katika vita vya Uhud akiwa na umri wa miaka hamsini na tisa.

> ***"Sikiliza kwa makini kuwa mimi pia kuanzia leo najiunga na dini yake na kusema kama asemavyo Muhammad saw ikiwa una uwezo basi njoo ushindane nami"***

Katika kitabu cha Sera Ibne Heshaam imeandikwa ya kuwa, "Mtume Mtukufu s.a.w akiwa amesimama karibu na maiti ya Hadhrat Hamza r.a alisema ya kwamba, "Ewe Hamza hakuna msiba mkubwa ulionifikia kuliko msiba wako huu, mimi sijawahi kuona mandhari ya kunihuzunisha kuliko mandhari ya leo kisha akasema ya kuwa Jibrili a.s amenijulisha ya kuwa Hamza Bin Abdul Muttalib r.a ametajwa kuwa simba wa Mungu na wa Mtume Wake katika mbingu saba. Imesimuliwa na Hadhrat Zubair r.a ya kwamba, "baada ya vita vya Uhud kwisha mama yangu Hadhrat Saffiya r.a alionekana kuja kwa kasi, Mtume saw hakupenda ya kwamba mwanamke yeyote aje kule na kuwaona mashahidi na maiti zao hivyo alisema ya kwamba, "mzuie mwanamke huyu" hivyo mimi nikamkimbilia kwa kumzuia lakini akanisukuma nyuma na kusema kuwa kaa mbali mimi sitakubali shauri lako lolote, mimi nikasema ya kuwa amri hii imetoka kwa Mtume s.a.w kwamba usizione maiti za mashahidi. Yeye kwa kusikia tu kauli hiyo akajizuia pale pale na kutoa nguo fulani alizokuwa amezibeba akasema kuwa nilikuwa nimezileta nguvo hizi za ndugu yangu Hamza kwani nimekwishapata habari ya kifo chake.

Huzur anasema ya kuwa, "huu ndio ule utii uliooneshwa na mama huyu ya kwamba licha ya kuwa na huzuni kubwa aliposikia tu kwamba Mtume s.a.w amemkataza kuiona maiti ya ndugu yake basi akajizuia pale pale. Huu ndio utii uliokamilika.

Mwili wa Hadhrat Hamza r.a ukavishwa kitambaa kimoja tu, wakati walikuwa wakifunika kichwa chake basi miguu yake ilikuwa ikibaki wazi na walipokuwa wakifunika miguu basi uso wake ulibaki wazi hapo Mtume saw alisema ya kuwa, "uso wake ufunikwe kitambaa na miguu yake ifunikwe majani. Siku ile Mtume saw alisalisha sala yake ya jeneza mara sabini pamoja na mashahidi wengine kwani kila mara maiti ya Hadhrat Hamza r.a ilikuwa ikiwekwa pale pale pamoja na maiti za mashahidi wengine.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema ya kuwa, "hao ndio wale watu ambao Mwenyezi Mungu Aliwaridhia nao wakamridhia Allah, waliokuwa wakiwakumbuka ndugu zao katika faraja na kuweka mbele yao hali yao ya zamani. Mwenyezi Mungu Aendelee kuziinua daraja zao juu kwa juu.

Hadhrat Kaab Bin Malik r.a aliandika juu ya kifo cha Hadhrat Hamza r.a ya kwamba, "macho yangu yanatiririsha machozi na yana kila haki ya kulia juu ya kifo cha Hamza r.a lakini kuna nini kitakachopatikana katika kulia juu ya kifo cha simba wa Mungu? Huyu simba wa Mungu (Hamza) asubuhi ile alipokufa shahidi, dunia ikalazimika kukiri kuwa huyu ndiye shahidi wa kweli.

Allah Aendelee kuziinua daraja za masahaba hawa na mifano yao ya kujitolea waliyoiacha, Waislamu waendelee kuikumbuka mpaka mwisho wa dunia. Na mifano ya wema ambayo walituachia Mwenyezi Mungu Atujaalie kuitekeleza katika maisha yetu. Aamin.

Jamaat Yabisha Hodi Kijijini Nungwe, Geita

Na Mwl Ramadhani Mahmood

Niliwasili katika kijiji jirani na Nungwe kiitwacho KAYENZE ambapo anaishi bwana Ally Tamimu. Manamo tarehe 21/7/2017 saa mbili usiku nikiwa mgeni wake kwa muda wa miezi miwili takribani. Usiku huo huo tulishauriana wapi tuanze mahubiri yetu, na baada ya mashauriano, tulikubaliana kuwa ni vyema sana kama tukianzia katika kijiji cha Nungwe. Hivyo kesho yake yani tarehe 22/7/2017 tulikwenda katika kijiji cha Nungwe asubuhi, na siku hii tulitumia zaidi kwa kujitambulisha na kuitambulisha Jamaat kwa viongozi wa Serikali ya kijiji cha kata.

Nao walihitaji niwapatie vitambulisho vyangu pamoja na barua zinazo nitambulisha na kuitambulisha Jamaat. Maana wakati ule kilikuwa ni kipindi ambacho mauaji yalikuwa yanaendelea kule Kibiti mkoani Pwani. Kwa sababu hiyo hao viongozi wa Serikali za vijiji walikuwa wameshapewa tahadhari juu ya wageni wanaoingia katika vijiji vyao na Serikali kuu.

Hivyo nilitoa vitambulisho vyangu pamoja na barua yenye usajili wa Jamaat hapo nchini Tanzania. Nao baada ya kujionea na kujiridhisha, muda huo huo wakasema hakuna shaka yeyote, karibu sana, endelea na shughuli zako nasi tutakusaidia. Hivyo tarehe 23/07/2017 ndio nilianza rasmi mahubiri na siku hiyo nilifanikiwa kupata familia moja ya kwanza kujiunga na jamati yenye jumla ya watu watano ambao hapo kabala walikuwa Wasuni familia ya mzee makerezia. Kisha tulifanikiwa kupata familia ya pili. Hii familia ya bwana Hassani Joseph Igulumuki ambao ilinipatia ushirikiano wa karibu sana kwa kutembea nami nyumba kwa nyumba tukienda tunahubiri Jamaat na Islam kwa ujumla.

Bwana Hasani alishiliki nasi nikiwa na bwana Ally Tamimu pia kwa siku tatu mfululizo na tuliongeza idadi kubwa ya Baiat, ndipo wao ilibidi waendelee na majukumu yao nami nikaendelea na mahubiri. Baada ya idadi yetu kuendelea kuongezeka, ndipo tulishauriana kupanga nyumba ili kukutana kwa ajili ya ibada na kuanzisha darasa. Ndipo bwana Hassani akaamua kujitolea kwamuda nyumba yake ili ibada ya sala na darasa vianze. Tuliendelea kusali katika nyumba ya bwana Hassani kwa kipindi chote ambacho tulikuwa bado kujenga msikiti hadi kufikia mwezi wa Februari 2018 tulipohamia sasa kusali ndani ya msikiti baada ya kukamilika.

UPINZANI ULIOJITOKEZA KUTOKA KWA WAKRISTO NA BAADHI YA WAISLAM WA KAYENZE

Baada ya kuingia kijijini Nungwe, nilikuta watu wa hapa wamegawanyika katika makundi matatu. Hapo Wakristo ambao wana makanisa makubwa na madogo takriban 10, pia walikuwepo Wapagani wengi tu, kadhalika walikuwepo Waislamu watano wa majina kwani hakuna walichokuwa wakitambua.

Hivyo baada ya kuona watu wengi wanasilimu na kuingia katika Jumuiyya, Wakristo walianza upinzani kwa kuhofia watu wao kuhama makanisani na kwenda msikitini, hivyo walianza kueneza uongo kwamba Uislamu ni dini ya Majini na kula utumbo wa maiti. Jambo ambalo halikusaidia kuwahofisha watu baada ya kutambua ukweli.

Kadhalika Waislamu (Wasuni) kutoka kijiji jirani cha Kayenze wao ndio walijaribu kuleta upinzani mkubwa dhidi ya Jamaat, kama kawaida yao baada ya kuona Jamaat imeingia kijijini hapo. Walianza kuwaendea watu waliojiunga na Jamaat na kuwaambia uongo kuwa, "hawa Wahmadiyya sio Waislamu safi, wana Mtume wao, Qur`an yao ina juzu 31, misikiti yao huwa imefungwa na haruhusiwi mtu kuingia kusali, wanatoa risiti pindi mtu akitoa sadaka kinyume na mafundisho ya Uislamu na mara hawana uwezo wa kujenga msikiti wanawadanganya tu na kuwapotezea muda wenu iliwaendelee kuchukua sadaka kutoka kwenu na kuendeleza biashara zao wazifanyazo. Hayo yote niliyatolea maelezo kwa wanajamati na walionyesha msimamo wa hali ya juu baada ya kuingia katika Jamaat. Hivyo Wasuni baada ya kuona kuwa wameshindwa kuwarudisha nyuma watu, waliwaendea viongozi wa Serikali ya kijiji na kata kuwaomba wanizuie kuendelea na harakati za dini kijijini Nungwe kwani wao kama Bakwata hawanitambui na sijapitia kwao. Hii ilikuwa ni mwezi wa 10/2017. Viongozi wa Serikali wakawaambia kuwa wao hawana uwezo wakuwazuia Ahmadiyya kwani wameona kwenye vyombo vya habari kuwa Ahmadiyya wamefanya mkutano wao wa mwaka kule Dar es salaam na mgeni rasmi alikuwa ni waziri mkuu Mh: Kasim Majaliwa.

Viongozi wakahoji "Sasa kama mgeni rasmi kwenye mkutano wao alikuwa waziri Mkuu, sasa sisi tutapata wapi uwezo wa kuwazuia.? Haya walinieleza wao wenyewe viongozi wa Serikali. Jamaa hawa wakashindwa hapa. Mara tena wakashauriana kwenda kwa Mkuu wa Polisi wa wilaya kwa kuwa nae ni Msuni, mtu wa Kigoma mwenzangu, wakakuta nae taarifa zangu anazo.

Basi jamaa hawa sasa hivi ni kama wamemwagiwa maji hasa baada ya Jamaat kujenga msikiti mzuri hapa Nungwe kwani wao walitangaza kuwa hatuna uwezo wa kujenga. Baada ya kuona tumejenga Msikiti mzuri na kivutio cha watu, sasa wanaanza kusema kwamba hawa ni Freemason ndio maana wamejenga msikiti mzuri hivyo. Ambao unazidi mbali sana wa kwao. Kwa kweli mfa maji haishi kutapatapa. Leo idadi ya wanajamaati hapa Nungwe inakaribia 300. Alhamdulilah

Ramadhan: Mwezi wa Funga

Kutoka uk. 1

uhilikishwaji wa Yerusalemu. Pia kuna funga za ziada kwa sababu husika, kama vile kutubia dhambi. Tunasoma: "Wakakusanyika huko Mispa, wakachota maji, na kuyamwaga mbele ya Bwana, wakafunga siku hiyo." Musa (as) alifunga mara mbili katika maisha yake kwa siku arobaini. Mara ya kwanza ilikuwa kabla ya kupokea amri juu ya Mlima, na pili, wakati wa kurudi kwake, alipowakuta Waisraeli wanafanya ibada ya sanamu.

Nilipokwenda mlimani kukaribisha meza za jiwe, hata meza za agano Bwana alizofanya nanyi, nikakaa mlimani siku arobaini na usiku arobaini, sikukula mkate wala kunywa maji; Bwana akanipa meza mbili za mawe ... Bwana akamwambia, Simama, ushuke haraka kutoka hapa; kwa maana watu wako uliowaleta kutoka Misri wamejidanganya wenyewe ... ... Basi nikarudi na kushuka kutoka mlimani ... Nikaanguka chini mbele za Bwana kama siku ya kwanza, siku arobaini na arobaini usiku: sikula mkate wala kunywa maji , kwa sababu ya dhambi zako zote ulizotenda ... " Katika Ukristo, tunasoma kwamba Yesu (as) alifunga siku arobaini akijiepusha na kula:

"Kisha Yesu aliongozwa na Roho kwenda jangwani ili akajaribiwe na shetani. Alipokuwa amefunga siku arobaini na usiku arobaini, baadaye akapatwa na njaa "

Yesu (as) alifunga kipindi hiki kirefu mara moja tu katika maisha yake. Labda hakujaribiwa na shetani tena. Katika Agano Jipya, funga yake ya siku arobaini imetajwa mara moja tu. Katika Ukatoliki, nyama pekee hairuhusiwi wakati wa kufunga. Mkate, siagi, mboga mboga, matunda, na aina zote za vinywaji zinaweza kutumiwa na saumu ikaendelea. Miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti, kufunga ni hiyari. Mkristo anaweza kufunga binafsi yake kama zoezi la kujidhibiti mwenyewe. Hakuna sheria za ulaji na makatazo na wakati na namna ya kufunga inaachwa kwa mtu husika.

Baada ya maelezo mafupi ya saumu katika dini nyingine, sasa tuje katika Uislamu. Kufunga kulianza mwaka wa 2 A.H. (Baada ya Hijrah), wakati aya hii ilipofunuliwa katika Qur'ani Tukufu:

Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wale wa kabla yenu ili mpate kumcha Allah"

Hii ikafuatiwa na amri iliyoiasisi Ramadhani, mwezi wa tisa katika Kalenda ya Kiislam, kama mwezi wa kufunga:

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito."

Kwa hivyo, Ramadhani ya mwaka wa 2 A.H. ikawa Ramadhani ya kwanza kufanywa kama mwezi wa kufunga. Kufunga ni lazima kwa Muislamu mtu mzima; wale ambao ni wagonjwa au wapo safarini wanapaswa kufunga idadi sawa siku nyingine, kulipizia saumu walizozikosa, wakipona au pindi safari yao ikimalizika. Wale ambao ni wagonjwa wa kudumu, wanakabiliwa na afya mbaya ya muda mrefu au wanakabiliwa na magonjwa ambayo hayatawawezesha kufunga kwa sababu za matibabu, wanashauriwa kulisha mtu maskini kwa kila saumu, ikiwa wanaweza kumudu kufanya hivyo. Sheria hii pia inatumika katika kesi ya wanawake wajawazito na wale wanaowanyonyesha watoto wao. Wale ambao wana safari za kudumu, kama madereva, walinzi wa treni, marubani n.k. hawana msamaha. Kwa madhumuni ya kufunga, hawahesabiki kama wasafiri, kama kusafiri ni sehemu ya kazi yao. Funga ya Kiislam ni huanzia tangu machweo hadi jioni. Waumini huacha kula na kunywa na aina zote za makutano ya kimwili kwa kipindi hiki. Kula daku kabla ya machweo husisitizwa ili kuepuka udhaifu usio wa lazima juu ya mwili na mara baada ya kuzama jua, muumini anaamuriwa kufungua saumu haraka bila kuchelewa. Mtukufu Mtume (saw) alisema "Watu watadumu kuwa na heri maadamu wataharakia kufuturu."



Quran iliteremka kwa mara ya kwanza mwezi wa Ramadhani

Kiini cha amri ya kufunga ni ***utii kwa Mungu***. Kwa maneno mengine, wakati Anaamuru 'kuacha', mtu haipaswi kula; na wakati Anaamuru 'kula', basi mtu anapaswa kutii bila kuchelewa. Zaidi ya hayo, mafundisho ya Kiislamu kuhusu kufunga ni yenye kuagiza zaidi na makali yakilinganishwa na imani nyingine. Kwa mfano, katika baadhi ya dini chakula kilichopikwa au kuokwa tu ndio hukatazwa, wakati mtu anaweza kula matunda mengi na kunywa na kiasi chochote cha maji. Katika imani fulani, nyama tu hukatazwa na milo nyingine yote inaweza kutumika kwa uhuru. Ruhusa hizi huhasiri madhumuni ya kufunga na kiini chake halisi, yaani, kupuuzwa kuacha kula na kunywa. Katika dini nyingine, kufunga ni lazima tu kwa viongozi na si kwa wafuasi wa kawaida. Hata hivyo, Uislamu huagiza kufunga kwa watu wazima wote, msamaha huhuhsika kwa wasioweza tu. Dini nyingine hutumia kalenda ya jua ili kuidhibiti saumu na matokeo yake, saumu zao daima huangukia siku zile zilizowekwa kila mwaka. Uislamu umechukua kalenda ya mwezi kwa lengo hili, maana yake kuwa saumu ya Kiislamu hufungwa mwaka mzima katika misimu tofauti wakati wa maisha ya muumini; hivyo mwaka mzima unahusishwa katika desturi hii takatifu.

Kuacha kula tu sio kusudio la Ramadhani. Mtukufu Mtume (saw) alisema: "Saumu ni ngao; hivyo anapofunga mmoja wenu, haimpasi kujiingiza katika mazungumzo ya hovyo wala kupiga kelele. Na mtu akimtukana au kupigana naye, basi aseme, 'Nimefunga saumu, nimefunga saumu!"

Kwa hivyo, saumu ni ngao ya kumlinda kutokana na uovu. Ikiwa mtu hujihusisha na maongezi au matendo yasiyofaa, kufunga kwake hakuna kitu. Mtukufu Mtume (saw) amefundisha: "Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mungu hana haja ya kwamba yeye aache chakula na kunywa kwake."

Mtu anayefunga anashauriwa kutumia muda mwingi kutekeleza wajibu wake kwa Mungu na viumbe Vyake. Anapaswa kutoa kipaumbele zaidi juu ya Sala tano za lazima pamoja na sala za daraja ya juu kama sala ya Tahajjud (baada ya usiku wa manane) n.k. Anapaswa kwa jitihada zake zote kuwasaidia maskini na wahitaji katika jamii. Kwa njia hii, atakuwa na uwezo wa kuzipata radhi za Mungu. Mtukufu Mtume (saw) amesisitiza juu ya sala ya Tahajjud wakati wa Ramadhani akisema: "Ambaye anasimama katika sala ya Tahajjud katika Ramadhani kwa imani thabiti na kwa nia ya kuzipata thawabu, dhambi zake zote za awali zinasamehewa."

Wale ambao hawawezi kumudu sala za Tahajjud katika Ramadhani, wanaruhusiwa kusali sala za Taraweh katika jamaa baada ya sala ya Isha (usiku). Hadhrat Umar (ra), Khalifa wa pili Kiislam baada ya Mtukufu Mtume (saw), alizunguka Madinah kila usiku ili kuangalia kuwa mambo yote yalikuwa sawa. Usiku mmoja, alipokuwa katika mizunguko yake, aliwaona watu wakisali msikitini baada ya sala ya Isha mwezi wa Ramadhani. Wengine walikuwa wakisali kwa jamaa na wengine peke yao. Akapendekeza wote wasali nyuma ya Imam mmoja, kwa hiyo alimteua Hadhrat 'Ubayy bin Ka'b (ra) kama Imamu wao. Kisha usiku mmoja alipokuwa kwenye mizunguko yake ya kawaida, aliwaona watu wakisali katika jamaa nyuma ya Imam. Alifurahia na akasema, "ni mzuri kiasi gani ubunifu huu" na akaongeza, "Lakini sehemu ya mwisho ya usiku ni bora zaidi kuliko sehemu hii". Alisema kwamba Tahajjud ni bora kuliko Tarawih.Mtukufu Mtume (saw) alisema: "Wakati mwezi wa Ramadhani unapoingia, milango ya mbinguni hufunguliwa na milango ya Jahannamu hufungwa, na mashetani hufungwa minyororo." Huu ni utukufu wa Ramadhani; kwamba mwezi huu kila njia za uovu zimezuiwa, ili mtu aweze kuufikia ukaribu na Mungu bila ya kizuizi. Hapa huibuka swali kutoka baadhi ya watu: Ikiwa mashetani wanafungwa katika Ramadhani, kwa nini maovu haya yanafanyika mwaka mzima, pia hutokea hata mwezi huu wa Ramadhani? Swali limejitokeza kama matokeo ya ukosefu wa kutafakari juu ya maneno halisi ya Mtukufu Mtume (saw). Anasema, "Wakati Ramadhani inapoingia." Inaingia wapi? Kwa wazi maana yake hapa ni kwamba wakati Ramadhani inapoingia ndani ya mioyo na roho ya waaminio, basi mashetani yao hufungwa. Mtukufu Mtume (saw) alisema, "Kila mtu ana Shetani ambaye anajaribu kumpotosha." Kwa hiyo, aliulizwa, "Na wewe, Ewe Mtume wa Allah?" Akajibu, "Naam; lakini shetani wangu ameshasilimu. "[Hadith hii inawafundisha waaminio wote ambao wanaruhusu Ramadhani kuingia ndani ya mioyo yao, kwamba mashetani wao bila shaka wamefungwa na hawawezi kuwadhuru waaminio hao, hata hivyo, wengine ambao mioyo yao Ramadhani haipati kuingia, huacha mashetani wao huru. Ndiyo sababu tunaona kwamba maovu pia hufanyika wakati wa Ramadhani kama vile yanavyofanywa katika miezi mingine. Katika Hadith Qudsi moja, Mtukufu Mtume (saw) alisimulia kwamba Mungu amesema, "Kila

Endelea uk 5

Wale ambao ni wa safari ya kudumu, kama madereva, walinzi wa treni, marubani n.k. hawana msamaha. Kwa madhumuni ya saumu, hawana hesabu kama wasafiri, kwa kuwa kusafiri ni sehemu ya kazi yao.

Ramadhan: Mwezi wa Funga

Kutoka uk. 4

kitendo cha mwanadamu ni kwa ajili yake, isipokuwa saumu; kwa maana ni kwa ajili yangu tu na mimi ndio malipo yake. "

Kama Mungu Asivyohitaji kula na kunywa, funga 'daima' ni yake, hata hivyo, mtu hawezi kuishi bila chakula, na anaweza kufunga kwa saa kadhaa tu. Wakati mwaminio, kutokana na upendo wake mkubwa kwa Mungu, anatamani kuwa kama Mpendwa wake na anajaribu kuacha kula, akizibeba shida kwa furaha, hivyo huvutia upendo wa Mungu. "Mimi ni malipo yake" inamaanisha mwaminio wa afungaye anampata Allah kama malipo ya kufunga kwake. Kwa matendo mema tofauti, mwaminio hupokea aina tofauti za neema; kwa kufunga anampokea Mungu Mwenyewe. Huu ni utukufu mkubwa wa Ramadhani. Mtukufu Mtume (saw) akiwaambia wafuasi wake alisema, "Enyi watu, umekuja mwezi mpya, mwezi uliobarikiwa." [Mtume saw] ametumia neno "Mubarak" (liobarikiwa). Neno hili limepatikana kutoka 'birkah', ambalo linamaanisha bwawa ambalo linapita maji ya mvua kutoka pande zote, hivyo Ramadhani kuwa mwezi 'Mubarak' inamaanisha kuwa mwezi huu ni mkusanyiko wa sifa zote njema.

Ramadhani ni shada kubwa la matunda ya kiroho linajumuisha ibada za faradhi na nafali, kufunga na matendo ya wema. ***Kuna hata ladha ya Hajj inapatikana***. Kuhusu Hajj tunajua kwamba "haipaswi kuwa na mazungumzo mabaya wala kosa lolote, wala mikwaruzano yoyote wakati wa kuhiji" (2:198); hivyo ndivyo ilivyo kwa Ramadhani: "Siku ambayo mtu yeyote anayefunga, haipaswi kujiingiza katika mazungumzo mabaya wala haipaswi kupiga kelele. Na mtu akimtendea vibaya au anapigana naye, anapaswa kusema tu, 'Mimi nina saumu, mimi nina saumu'. Hapa kuna kauli nyingine ya Mtukufu Mtume (saw) ambayo inavuta nadharia zetu. Alasema, "Naapa kwa Yule ambaye uhai wa Muhammad umo mikononi mwake kwamba, Harufu ya kinywani mwa mfunga saumu ni bora zaidi mbele ya Mungu kuliko harufu ya miski". Khaluf ni harufu mbaya. Kuna aina mbili za harufu mbaya inayotoka kinywa kimoja:

1. Harufu inayosababishwa na mabaki ya chakula kwa kutosugua kinywa baada ya milo. Hii sio harufu iliyotajwa katika Hadithi, kwa sababu uchafu huu unachukiwa katika Uislam. Mtukufu Mtume (saw) amesikiwa kuwa alisema, "Safisha meno yako, safisha meno yako, usije kwangu na meno machafu". Alifundisha kwa msisitizo kusafisha kinywa baada ya kula. Alisafisha kinywa chake mara kadhaa kwa siku - si mara mbili tu - na fimbo ya kusafishia (miswak). Hata wakati wa saumu, mara nyingi alikuwa akisafisha kinywa chake kwa 'miswak'. Alisema, "Kati ya tabia bora za mtu kufunga ni kusafisha kinywa na 'miswak". Mbadala wa miswak ni kusafisha meno kwa kutumia mswaki wa kawaida na dawa ya meno, hivyo mtu anayefunga anashauriwa kusafisha kinywa mara kwa mara wakati wa kufunga.
2. Aina ya pili ya harufu isiyokubalika inayotoka kinywani haisuhubiani na uchafu. Kwa mujibu wa Kiarabu, "Khuluf ni mabadiliko ya harufu ya kinywa yanayosababishwa na kuchelewa kula." Kwa hiyo, Arnold Ehret anaandika katika kitabu chake *Rational Fasting*: "Kila mtu mwenye afya au mgonjwa hupata ulimini ute unukao punde anapopunguza kula au kufunga. Hii hutokea pia kwenye ute wa ukuta wa tumbo ambayo ulimi ni nakala yake halisi."

Kwa sababu ya kufunga, ulimi na tumbo vinaathirika; wakati ulimi unaondolewa harufu hii mbaya kwa kusafisha mara kwa mara, hakuna kitu kinachoweza kufanywa kuhusu harufu kutoka tumboni na hii ndiyo harufu ambayo imetajwa katika Hadith. Sio kutokana na uchafu badala yake ni matokeo ya kuacha kula. Kama mwaminio anateseka na hili ili kuitii amri ya Mungu, harufu hii inakuwa yenye kumpendeza zaidi Mungu kuliko harufu ya miski. Hebu fikiria mavazi yenye kunuka ya yule anayejitosa mtaroni haraka ili kumuokoa mtoto wa mtu ambaye aliangukia humo kwa ajali. Fikiria jinsi mavazi yao yenye kunuka yanavyokuwa mazuri kwa mama wa mtoto!



Mtukufu Mtume (saw) alitumia ***miswak*** kusafisha meno yake, hata wakati wa saumu

Maana ya Neno 'Ramadhani'

'Ramadhani' imechukuliwa kutoka kwenye mzizi Ramd, ambao linamaanisha moto uchomao. Mtukufu Mtume (saw) alifundisha, "Ramadhani imepewa jina hili, kwa maana huzichoma dhambi zote." Mtu hufunga akipitisha Ramadhan akikidhi masharti yote ya mwezi ili kuibuka na takasiko la kiroho. Ramadhani huenda kuwa imetokana na Ramd Al-Nasl, ambayo ina maana 'kuweka kichwa cha mkuki kati ya mawe mawili msawazo na kukipiga vizuri ili kukinoa.' Katika suala la kufunga, mawe mawili msawazo ni asubuhi na jioni, katikati yake ambapo, roho ya mfungaji hupigwa na maumivu ya njaa na kiu kikubwa na kwa hiyo huimarishwa. Machweo na mawio ni laini, kwayo waaminio hupata kula na kunywa katika nyakati mbili hizi na hivyo kwa nafsi iliyo kali, waaminio wanaweza kushinda mashambulizi ya Shetani. Tena, Ramadhani inaweza kuwa imetokana na Ramada Al-Tair, ambayo inamaanisha kuungua kwa tumbo la ndege kutokana na kiu kikubwa. Hivyo, ndege hupaa akihaha katika mielekeo tofauti akitafuta maji ili kukata kiu yake. Vivyo hivyo katika Ramadhani, mwaminio, ambaye ni ndege wa kiroho, huwa hatulii kutokana na kiu cha mapenzi ya Mungu. Anajitahidi sana kutafuta maji ya mapenzi ya Mungu na husahau kula na kunywa na hujiingiza katika vitendo tofauti ili kufikia lengo lake. Hatimaye, Mungu humpa mapenzi Yake na huyo mwaminio hupata ridhiko lakiroho.

Itikaf - Siku 10 katika Kujitenga

Itikaf inamaanisha kujitenga. Katika istilahi ya Kiislamu, inamaanisha kujiondoa katika masuala ya kidunia na kujishughulisha na kumkumbuka Mungu katika siku kumi za mwisho za Ramadhani, haswa kuishi msikitini. Mtu hapaswi kutoka isipokuwa kwenda haja au kuoga. Wakati huo hutumiwa katika kusali, kuomba, kusoma Qur'ani Tukufu, na kutafakari juu ya maana yake ya ndani. Wakati mtu anaweza kulala kidogo wakati wa mchana au usiku ili kujiweka murua, wakati mwingi unapaswa kutumiwa kukumbuka Mwenyezi Mungu. Mtukufu Mtume (saw) alikuwa akiingia katika mahala pake pa Itikaf siku ya 20 ya Ramadhani, baada ya sala ya Alfajir. Itikaf hukamilika kwa kuandama kwa mwezi ujao, Shawwal, baada ya siku 29 au 30 za Ramadhani.

Lailatul-Qadr (Usiku wa Heshima)



Katika siku kumi za mwisho za Ramadhani, kuna usiku fulani kati ya usiku usio wa kawaida wa kipindi hiki hutokea kinachojulikana kama Lailatul-Qadr kwa istilahi ya Kiislam. Inaweza kuangukia siku ya 21, ya 23, ya 27 au ya 29 ya Ramadhani. Usiku huu umejaa baraka kemkem kwani huu huonekana kuwa kilele cha Ramadhani na maombi yanakubaliwa kwa urahisi sana usiku huu. Hadhrat 'Aishah (ra), mke wa Mtukufu Mtume (saw), alimwambia Mtume (saw) "Niseme nini, nikiwahi kutambua usiku fulani ndio usiku wa heshima (Lailatul-Qadr)?" Mtukufu Mtume (saw) akasema: "Sema hivi, Ee Mola wangu! U Msamehevu, Wapenda kusamehe, basi nisamehe". Mwaminio ambaye anatimiza matakwa na mahitaji yote ya Ramadhani kwa juhudi kamili na kwa dhati anaweza kufanikiwa kupata usiku huo na ni hisia kali ya kiroho ya waaminio ambayo inamshawishi ya kuwepo kwa usiku wa baraka.

Mafunzo ya Ramadhani

i Mtu anayefunga anahisi maumivu ya njaa ndani ya tumbo kwa mwezi kamili na huja kujua kwa vitendo kwa kiasi kikubwa mateseko ya masikini katika jamii. Hii inamuhimiza kuwasaidia masikini kwa moyo wote akiwa na uzoefu binafsi wa shida yao kwa uzito stahiki.

ii Kupata kifungua kinywa wakati usio wa kawaida kabla ya alfajiri inaonekana kuwa vigumu sana mwanzoni, hata hivyo desturi hii humfunza mtu anayefunga kukabiliana na hali isiyo ya kawaida wakati akiwa katika mgogoro anaweza kula chakula nyakati zisizo za kawaida pamoja na misukosuko mingine katika hali ya kawaida ya maisha.

iii Mtu anayefunga hujiepusha hata na vitu vya halali wakati wa Ramadhani kwa ajili ya kupata radhi ya Mungu, kwa hiyo inakuwa rahisi kwake kuepuka vitendo vya kinyume cha sheria kwa ajili ya Mungu.

iv Saumu inafundisha kwamba kwa kufanikisha malengo ya juu, mtu anahitaji kuweka juhudi kubwa na ya kweli.

Tunamwomba Allah Atuwezeshe sisi sote kufunga Ramadhani, kukidhi masharti yake na kutekeleza vigezo vyake vyote ili kuipata radhi ya Mungu, Amin.

MCHANGO WA ZAKATUL FITRI, EID FUND NA FIDYA

Wanajumuiya wote wanafahamishwa kwamba:

- **Mchango wa Zakatul Fitri mwaka huu ni Tsh. 3,000 kwa kila Mwanajumuiya.**
- **Mchango wa Eid Fund ni Tsh. 3,000 kwa kila mkuu wa familia au mwenye kipato binafsi.**
- **Fidya ni Tsh. 2,500 kwa siku (75,000 kwa mwezi) kwa wale walio na dharura ya Kisheria ya kutokufunga na wanawajibika kutoa fidya.**

Tujitahidi kutoa kwa wakati.

Bustani ya Washairi

RAMADHANI KAWASILI

1 Alihamudulillah, namshukuru Muumba,
Natamka watallahi, kwa haki alituumba,
Na mukusudi sahihi, hakika aliyapamba,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

2. Kulima huko nasema, kwa kufunga Ramadhani,
Amri hii kasema, ndani yake Kuruani,
Waislamu kauma, tutimize ya zamani,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

3. Kilimo hicho nanadi, Mola ametujalia,
Tupande humo mahindi, mavuno kujizolea,
Yakiotapo mahindi, matokeo kuyajua,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

4. Enyi mlioamini, Mola katuelezea,
Kuifunga Ramadhani, ni amriye katoa,
Ni lazimisho la dini, kila mumini ajua,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

5. Kufunga ndugu jamani, Ucha Mungu huchangia,
Mwezi huo Ramadhani, dhambi hutuondolea,
Juhudi tuweke ndani, maombi kuendelea,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

6. Katujalia Rabuka, Saumu katuridhia,
Maovu kuyaepuka, thawabu kujitwalia,
Na Shetani huondoka, kuiwacha wazi njia,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

7. Kulima huko hakika, kwahitajia mbolea,
Samadi naitamka, ni maombi kwa Jalia,
Wahitaji kuinuka, usiku kumlilia,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

8. Hii ni bahati yetu, muhula kuufikia,
Tumeuona kwa yetu, macho katuangazia,
Huyu Muumba ni wetu, mapenzi katutakia,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

9. Kituoni nimefika, kalamu chini natua,
Waumini natamka, nawaombea Jalia,
Mola aliyetukuka, atujalie jamia,
Ramadhani kawasili, Waislamu tulime.

Harun R. Bundala,Tabora.

KARIBU WETU MGENI

1. Bisimillahi ya kwanza, naingia mtamboni,
Jinale liwe la kwanza, Rabuka ndiye Manani,
Ramadhani inaanza, barakayo ya kifani
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

2. Ramadhani imeanza, waaminio fungeni,
Wala msione manza, Mola kaweka funguni,
Imani iwe ya kwanza, sambamba na viungoni,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

3. La usiwe kama panza, dunia kuitamani,
Onyo hilo si la anza, matamko ya Manani.
Kale yetu walianza, matamko ya Manani,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

4. Mola wetu kahimiza, sisi sote tu tufungeni,
Hesabuye huianza, zitimiye thelathini,
Hizo siku za aziza, timilifu za mwezini,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

5. Nguzo hiyo si ya kwanza, nne nazo zipembeni,
Zote zakutekeleza, pate ingia peponi,
Rabuka kazipambiza, bila shaka asilani,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

6. Ramadhani ikianza, ibilisi kizimbani,
Mola huwa ni wa kwanza, Pepo kututakieni,
Binadamu hujibeza, hawakumbuki hisani,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

7. Mwezi siwe wa simanza, Rabuka tupe imani,
Baraka kuzisambaza, kuning'iniya pingoni,
Shetani ka kibaraza, siku zote thelathini,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

8. Ibada iwe ya kwanza, siku zote thelathini,
Shetani kumfukuza, asitutie dhambini,
Rabana lete mwangaza, tukaingie peponi.
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

9. Wazamani walianza, kuifunga Ramadhani,
Hao Mungu kuwakweza, kuingia baridini,
Nasi kwao kujibanza, laiti tuwe makini,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

10. Mola wakamtukuza, na siye tuwe mbioni,
Nuru ipate angaza, kwetu siye nafusini,
Imaniyo kutujaza, natufunge kwa amani,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

11. Rabi wetu uliojaza, mbinguni na aridhini,
Rehemazo kama chaza, kaufu twishe begani,
Wewe Mola wa baraza, hukumuyo si utani,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu

12. Hapo nalachameza, kalamu nawekachini,
Saumu itapekaza, jioni tufuturuni,
Mola pokea ibaza, na ututie funguni,
Karibu wetu mgeni, Ramadhani mtukufu.

H.A. Makando,Tanga.

HUISHI WATU WACHACHE

1. Bismillahi naanza, jina la Mola nichuche,
Si neno la kupuuza, tumhimidi tumche,
Ulimwengu mtengeza, Muumba watu na miche,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

2. Iwapo limekukwaza, jambo moja likuchoche,
Sana limekutatiza, wape wenziyo wakoche,
Vizuri watakujuza, wanaojuwa mbalache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

3. Nataka kukutuliza, na wasiwasi uache,
Nyumba hiyo si ya giza, wala umeme wa cheche,
Baiti ya kugeuza, khulka mbaya tuache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

4. Basi akili tuliza, hauwezi upupuche,
Tupo tutakuongoza, upate mwanga mwangache
Kilicho kukukingiza, takusomesha abeche,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

5. Kama ulivyo dokeza, siyo nyumba ya mikoche,
Ya mawe ya kukereza, kwa kokoto si miloche,
Kwa ndani inapendeza, na nje iangaache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

6. Nyumba ya akhi Miriza, si danguro si maguche,
Ni ya dini kueneza, ni kazi ngumu si kweche,
Pahitajika mwangaza, wa Imani si ngangache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

7. Tarekhi inaeleza, haijuzu tuikache,
Mitume walitangaza,ujumbe ule mbweleche,
Kionesha miujuza, walokubali wachache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

8. Pamwe kufanya mujiza, kila aina iliche,
Manabii wake Azza, hukanwa ka kamba-koche,
Na waliyojiingiza, si wengi bali wachache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

9. Quruani yaeleza, hali ya Nuhu mkiche,
Kisa haukikijaza, usomile kimacheche,
Nuhu alowaingiza, marekebuni wachache,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

10. Hisitori yaongeza, wapo mitume fufuche,
Wakazi hawakuweza, kupata japo kangache,
Kila mmoja kibeza, hata wahedi situche,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

11. Wingi hujapatiliza, kuwa batili uchache,
Uchache hauwi kiza, hata mchwa wapukuche,
Kweli nyumba ya mwangaza, japo washike wapeche,
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

12. Kama wingi ni mwangaza, wa ukweli kamba kuche,
Manaswara watumeza, na waso dini idache,
Sasa ninakuuliza, nyumba zao tusiache?
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

13. Tama zao zimejaza, wakazi wala mbuguche,
Tuziite za mwangaza, au za giza tuchoche?
Wakazi ilowajaza, ni wengi ama wachache?
Huishi watu wachache, nyumba za waja wa Azza.

Al-Ustadh Khamisi S.S. Wamwera,
Kimbangulile, Mbagala Rangi Tatu,
Kata ya Charambe, Dar es Salaam.

KARIBU WETU AMIRI

Salamu Aleikumu, wapenzi na wanachama
Sheitani Warajimu, kwanza aende mrama
Katika hizo salamu, za furaha na heshima
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Pole kwa safari yako, tabu nyingi majiani
Umefata ndugu zako, Mola akupe hisani
Halitakosa ukoko, jungu kubwa kwa yakini
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Jumuiya sasa kubwa, kama unavyo iona
Kwa wote wako kundini, tisa iwe namba wani
Wasije tena kusombwa, mawimbi ya baharini
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Mola akupe rehema, Baraka pia Amani
Utembee nchi mzima, uwaone waumini
Tabora hadi Dodoma, kadhalika visiwani
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Urambo hadi Kalihama, Nguruka umeiona
Nguruka nimeisema, Kigoma umo njiani
Akujalie Karima, Chaudri wetu rubani
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Kwako hakuna lawama, kwakazi nambari wani
Kwakazi unajituma, hakuna chako kifani
Hongera tena nasema, uimetutia imani
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Wendako tunakutuma, kwa ndugu waloamini
Kamwe wasirudi nyuma, ufike hadi kusini
Mwindaji usijekoma, unaranda msituni
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Wapigane na dhuluma, dunia iko mwishoni
Pole kwa wacheza ngoma, wao wameshindwa dini
Nguruka hadi Kigoma, hata mlo Kinondoni
Karibu wetu Amir, Mbashiri Tanzania.

Moshi Mohamed, Nguruka.

MKO WAPI WASHAIRI?

Mabingwa wetu malenga, watunzi wa mashairi,
Wa visiwani na Tanga, tunaomba mistari,
Mashairi yenye mwanga, ya kutoa ubashiri,
Mko wapi Washairi, mbona hamuonekani.

Tunawaomba kutunga, beti tamu ja sukari,
Za shetani kumtwanga, na kueneza mazuri,
Twawasubiri nyakanga, mezani kwa Mhariri,
Karibuni Washairi, kwenye yenu bustani.

WATOTO! HAPA NI KWA AJILI YENU

Jee unaijua Shahada ya Kiislamu?
Shahada ya Kiislamu ni kutamka:
Laa Ilaaha Illa Llahu, Muhammadu Rasuulu Llah.
Maana yake ni kwamba:
Hakuna anayepaswa kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu; Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.
Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Pia ndiye Aliyetuumba sisi sote. Yeye anatupenda sana na ndiye anayetupatia kila tulichonacho.
Hivyo na sisi tunatakiwa tumpende sana na tumuabudu yeye tu.
Mtume Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu aliyetumwa ili kuwafundisha wanadamu wote jinsi ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.
Wakati linapotajwa jina la Mtume Muhammad s.a.w. tunatakiwa tuseme: Swalallahu Alaihi Wassalaam. Maana Yake Rehema na Amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.
Kutamka maneno hayo kunaitwa kumsalia Mtume s.a.w.

Wazazi na walio wakubwa wawaongoze watoto katika kutamka na kurudia maneno hayo kila mara. Msisitizo maalum uwekwe juu ya watoto wa waqfu Nau

CHEMSHA BONGO



Kwenda Kulia
1. Mwenyezi Mungu mmoja
6. Mahubiri
8. Kiungo cha pilau
10. Hali ya utulivu
12. Nyumba ya Allah
14. Umoja wa Wahandisi wa Kiahmadiyya
16. Uelewa/Fahamu/Maarifa
17. Kundi
18. Watoto wa kiume
20. Mienendo ya Mtume s.a.w
21. Nguo maalum ya kuhifadhia mwili
22. Utamaduni tangu na tangu
23. Kujitahidi katika njia ya Allah

Kwenda Chini
2. Ibada kwa wenye uwezo
3. Mwana mkuu wa Ibrahim
4. Watumishi wa Ahmadiyya
5. Mashauriano
7. Mwongozo kwa wanadamu
9. Mwakilishi wa Huzuur nchini
11. Tindikali
13. Shuka mbili
15. Mwanzo
16. Kitu alichokabidhiwa mtu akitunze
18. Kukubaliana na sera/imani fulani
19. Ibada ya Pamoja
20. Ibada kuu

TAFUTA MANENO

Kuna maneno Ishirini na nane (28) katika jedwali hapo juu. Yatafute kwa kuyazungushia na kalamu ya risasi (Penseli)

J	Y	C	L	H	M	X	F	Z	K	C	K	W	M	M	D	W	L	H	R	K	Q
K	G	G	R	A	G	Y	B	R	D	A	B	D	U	L	L	A	H	N	Z	P	K
M	B	D	L	C	Z	R	K	W	R	Y	M	J	Z	L	L	J	N	L	N	H	V
Y	G	S	D	H	P	R	D	J	R	M	Y	H	H	A	F	I	D	H	C	K	T
V	I	B	C	A	C	Y	T	L	F	D	P	K	A	X	H	S	N	B	B	K	I
L	M	R	R	D	L	R	Z	M	R	B	A	H	J	D	L	J	A	H	K	L	B
C	H	L	T	I	T	K	T	C	J	J	S	X	P	R	H	S	N	L	I	Y	T
G	V	I	F	T	K	R	C	M	I	L	A	X	L	M	F	R	U	D	A	T	N
R	Q	R	J	H	T	T	R	D	T	Q	H	C	H	T	T	G	A	N	N	T	A
F	X	Q	A	A	V	T	A	R	T	Y	A	V	M	F	P	R	W	T	N	B	D
Q	M	Z	B	M	B	H	N	Y	R	F	B	Q	U	B	L	X	P	R	R	A	H
Z	N	F	U	M	K	Y	L	M	L	N	A	P	B	R	J	G	Z	P	X	Z	A
R	P	W	B	K	J	A	M	A	A	A	M	L	A	R	A	B	U	W	A	P	N
C	Q	J	A	D	Q	C	T	G	N	T	B	R	H	R	Y	K	T	H	R	G	A
Q	W	I	K	Z	T	X	R	T	Q	C	N	A	A	N	M	Y	S	N	H	M	D
X	H	B	A	W	T	K	M	L	X	J	B	Z	L	W	M	I	V	N	Z	W	I
R	A	R	R	T	D	N	V	P	X	A	H	M	A	D	A	M	A	Q	J	N	W
P	S	A	Y	R	T	J	H	Z	A	V	T	M	Z	I	W	J	F	M	I	L	H
Q	I	H	V	Q	J	A	M	K	W	L	B	Y	F	N	H	G	Q	D	I	Y	P
N	D	I	J	C	L	A	T	N	N	R	K	Z	R	K	M	S	R	Z	F	N	G
H	I	M	M	L	R	P	M	M	F	Z	C	M	A	D	I	N	A	Z	Q	T	A
N	K	F	A	L	B	T	W	A	D	C	L	X	X	T	N	T	T	N	N	C	B
R	N	Q	J	P	L	J	C	T	A	T	K	R	N	M	U	H	A	M	M	A	D
K	F	T	Y	A	T	H	R	I	B	T	V	H	Z	M	K	Y	N	Q	K	J	Z

JE WAJUA?

Moja kati ya njia bora kabisa za kukikumbuka kitu ni kukielezea kwa mwingine.

Utafiti unaonyesha kwamba unapompashamtuulichojifunza,huenda ukawa na kumbukumbu za kitu hicho kwa muda mrefu zaidi kuliko ukakisoma tena hicho kitabu au maandishi.

Wakati ubongo wako unazichambua kumbukumbu, huzitunza zile muhimu zipatikane kiurahisi zaidi, kwa sababu huifanya taarifa ile uliyomwambia mtu mwingine ni ya muhimu sana.

Hivyo mnaaswa kurahisisha kujifunza kwenu kwa kusoma pamoja na wengine..

Kuepusha Migogoro na kujenga Mahaba katika Ndoa

Kutoka toleo Lililopita

Ndugu wasomaji,

Wanawake watarekebishika zaidi kupitia matendo ya wanaume. Na sisi wanaume iwapo tutamuelekea Allah na kuwa wenye taqwa, basi Allah Atatunusuru kwa mapungufu yetu na makosa yetu madogo madogo. Na ifikie hatua kwamba hawa wake zetu hata kama wajaribu kutafuta makosa madogo madogo kutoka kwetu sisi waume zao basi wasipate hata chembe ya makosa. Na iwapo kweli hawatopata na kubaini makosa madogomadogo kutoka kwetu sisi wanaume, basi hakika wake zetu watabadilika na kumuelekea Allah mtukufu ambapo kiujumla itanawirisha hali nzima ya nyumba zetu Insha'Allah. Wanawake wanapojawa hasira mara nyingi huongea sana, huropoka, huwa wanashindwa kujizuia na anaweza kumuhadithia yeyote awaye mbele yake juu ya mambo yao ya ndani, huku akijisahau kuwa hapo anaidhalilisha nyumba yake na mume wake. Yatupasa tuikumbuke pia hadithi ya Mtume SAW iliyosema "aliyefaulu ni yule aliyekaa kimya" Tusizishike tabia hizo njema za kukaa kimya pale hali ya mizozo na kutokuelewana ndani ya ndoa zitokeapo, maana Mtume SAW ametuambia tutafaulu kwa kukaa kimya. Tuepuke khulka mbaya, hakika hizo si khulka njema kwetu, khulka mbaya hazina faida kwa maisha yetu haya ya ndoa. Iwapo ipo migogoro na baadhi ya mambo ambayo hayakufurahishi ndani ya mji wako, basi si vema kuita kikundi cha watu na kuwahadithia ili uombe ushauri, kwamba uwalalamikie ili wakusaidie, hao marafiki si wote wakutakiao kheri katika nyumba yako. Bali tujue fika ya kwamba mpaka ndoa inafungwa basi walikuwepo washenga na mawalii wa ndoa hiyo, watumiwe vema hao sambamba na kuwashirikisha wazazi. Pale muonapo hali isiyofikia tamati njema, basi ndipo iwe ni hatua ya mwisho kuufikia uongozi wa Jamaat na kuomba msaada wa shauri, shauri ambalo linapowasilishwa katika uongozi wa Jamaat basi tayari jambo hilo liwe limepitia ngazi hizo ili kuleta urahisi wa hekima ya muafaka mwema na muongozo mwema kutoka Jamaat.

Qur'ana inatuambia pia kuwa ikiwa kumetokea hali ya kutokuelewana, basi njia salama kwenu ni kushika suluhu iliyo njema. Suluhu njema inapowapata wanandoa, hakika huwa ni ishara njema ya kwamba Allah anawahurumia wanandoa hao, anawapenda wanandoa hao na anawaimarisha ili wafikie hali ya kilele cha lengo la kuumbwa kwao ambacho ni taqwa. Na katika suluhu hizo zote zinazofanywa, basi ziwe ni suluhu zinazoridhiwa kwa dhati na nafsi zetu ili zisibakishe chembe yoyote ya ubakhili ndani ya nafsi ya mmoja wao katika kufikia hilo. Fundisho kubwa ambalo tunakumbushwa ni kuwa walau mume kujiepusha na hali ya ubakhili bali pia mke apunguze tamaa.

Kuna mwanazuoni mmoja wa Kiislamu alipata kusema na kutoa nasaha fulani kwa mke, wake zake nami naomba niwawasilishie ili itusaidie. Alisema…… Ewe mpendwa mke uliyetangulia kuolewa na kumkaribisha mke wa pili au watatu au wanne. Tambua ya kwamba kuolewa kwako na kuwa mke wa kwanza kwa mumeo haikufanyi uwe ni malkia kwa wake wenzako. Hivyo usiwashurutishe kimamlaka, hao si walio chini yako, hao si watoto wako, hao si wajukuu zako, hao si watumwa kwako, na hao si sehemu ya wajakazi wako. Ninyi wote mmekuja kutoka sehemu tofauti kuja kuujenga mji mmoja wa mume wenu, nyumba ya mume wenu hapa duniani. Hivyo usije kufanya maajabu na viroja vya maisha kwa wake wenza wenzako, si dhambi hata kidogo wao kuolewa na mume uliyeanza nae maisha. Kujaaliwa kwako kuwa ni mke wa kwanza kuolewa na mumeo haina maana yoyote isipokuwa ni kutangulia tu, lakini haikupi mamlaka yoyote dhidi ya wake wengine. Hakuna Aya yoyote au Hadithi yoyote isemayo kuwa mke wa kwanza ni MKUBWA AU NDIO MWENYE BAHATI NJEMA ZAIDI KULIKO ALIYEMFATIA. Hata kama wewe ni mkubwa kiumri kuliko waolewaji waliokufatia, hailazimishwi wao ndio wakuheshimu wewe. Bali ni jukumu jema kwenu wote kuheshimiana baina yenu. Hata kama wewe mke uliyetangulia umejaaliwa kuwa ni Profesa ilhali mke mwenzako yeye si msomi kabisa (yaani mbumbumbu), lazima muheshimiane kwa stahiki sawa kuwa ninyi nyote ni wake na mmeolewa na mume mmoja. Hakuna mahala ilipoandikwa na kudaiwa kuwa eti kupata hadhi ya daraja la shahada kielimu au utajiri wa mali ulionao basi hiyo ndio ikufanye wewe kuwa ni mke bora zaidi ya mwenzako, bali imani na daraja mbele ya Allah ndio kipimo bora zaidi na ikifuatiwa na tabia. Katu ewe mke uliyetangulia kuolewa isikufanye ushindane na mke mwenzio au umkandamize, jiepushe na kulaumu na kuwanung'unikia watoto wa mwenzako, na katu jiepushe kupaza sauti koridoni na vibarazani mwako huku ukipayuka kwa kumsema mke mwenza mwenzio "aah huyu yeye ni mke wa pili tu na hivyo yeye ni kama samani tu ya ndani ya nyumba yangu". Ewe mke wa kwanza, usianzishe na usiwe ni chanzo cha migogoro, magomvi na misukosuko ndani ya nyumba kwa kuwa tu mke mwenzako ni mkimya, mtulivu na asiye na makuu au yeye ni maskini kabisa, mpofu. Chonde usiwe ni sehemu ya chanzo, jilinde na jiepushe. Jiepushe kuonyesha aina yoyote ile ya dharau kwa mke mwenzio hasa pale itokeapo umeambatana pamoja na mume wenu, jishushe na usionyeshe hata chembe ya dharau kwa mke mwenzako. Enyi wake wenza, jifunzeni kuishi kwa amani na kuepusha mivutano. Huyu ni mume wenu wote. Je mnadhani mtaishi milele katika maisha haya mafupi huku mkilumbana na kuanzisha hali za chuki miongoni mwenu shauri ya kugombea mume wenu? Je, hivi mnajiuliza ya kwamba huyu mume wenu ambaye leo hamuelewani baina yenu kwa kumgombea, kwamba huenda hii leo ataitikia wito wa Allah na kuiaga dunia, mnalijua na mnalikumbuka hilo? Na je, iwapo huyo mume wenu mnayemgombea huku amani ikiwatoka ya kwamba hii leo amefariki na kutoweka juu ya ardhi hii ya dunia, mtaendelea kugombana na kutokuelewana? Yapasa mtafakari sana. Kwani inawezekana wewe ambaye ndio chanzo cha misukosuko ndani ya nyumba huenda ndio ukawa wa kwanza kutangulia mbele ya Allah na wala usiishi miaka mingi hapa duniani kama ufikiriavyo. Itakuwaje wanao wachanga uliowaacha hapa duniani wanaanza kulia wakihitaji kunyonyeshwa, ni nani atakayewanyonyesha na kuwasimamia watoto wa mumeo? Hapo wewe hautakuwepo duniani na wala hautatoa msaada wowote kwa mwanao mchanga uliyemuacha akihitaji kunyonya. Leo hautakuwa na uwezo wa kugombana na mke mwenzio na kuringishia watoto mbele ya mume wenu, leo hautatoleana maneno ya kuudhi na mke mwenzio juu ya hadhi tu kwamba eti mimi nina watoto hivyo nastahili uzito kwa mume wetu, au mimi nina mali au mimi nimejaaliwa elimu zaidi. Yote hayatakuwepo na yatayeyuka. Leo hayapo tena mashindano uliyokuwa ukiyafanya dhidi ya mke mwenzio juu ya mume wenu. Waila inawezekana yule mke mwenzio ambaye maisha yote ulikuwa ukimuudhi, ukimdhihaki, ukimsengenya, ukimnyanyasa na ambaye ulikuwa ukimringia, sasa ndio atakuwa ni mlinzi na mlezi wa watoto wako uliowaacha, akiwapikia kila siku, akiwapa na akiwaonyeshea upendo wa dhati, huku akiwanepisha kila mara pale wajisaidiapo maana ni wadogo na hawajiwezi. Nyakati hizo ukumbuke kuwa wewe hautakuwepo juu ya ardhi hii tunayoikanyaga leo."….mwisho wa nukuu hiyo ya mwanazuoni huyo wa Kiislamu.

Enyi akina baba wapendwa na ambao mmejaaliwa kuoa mke mmoja na kuoa mke zaidi ya mmoja, naomba tuisikilize aya hii na tuitafakari kwa kina namna ambavyo inatukumbusha ili tuhuishe upendo na mapenzi kwa wake zetu ndani ya nyumba zetu. Al Qur'an inasema: ''Nanyi hamuwezi kufanya uadilifu uliokamilika baina ya wake, hata kama mngependa namna gani. Kwa hiyo msiegemee moja kwa moja kwa mke mmoja isije mkamuacha mwingine kama aliyeangikwa yaani (asiyehudumiwa na asiyeangaliwa). Lakini kama ninyi mkijirekebisha na mkijilinda na uovu basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.''

Daima tukumbuke kuwa, Allah mtukufu ametujaalia mfano wa kiumbe wake Muhammad Mustafa SAW pale alipotueleza ndani ya Qur'an kuwa "Mnao mfano mwema wa Mtume Muhammad SAW'.

Na kisha hadithi nyingine inaendelea kutukumbusha sisi wanaume Iliyosimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah ra ya kwamba Mjumbe wa Allah SAW alisema: Watunzeni wanawake vizuri. Kwani mwanamke ameumbwa kutokana na ubavu (yaani tabia yake imepindamana). Na mfupa wa ubavu huwa unapindamana zaidi sehemu ya juu. Mkijaribu kuunyoosha mtauvunja. Na mkiubakiza katika hali yake utabakia katika hali ya kupindamana (na mtafaidika nao). Basi waangalieni wanawake vema.

UKUMBUSHO MUHIMU KWA WANANDOA WENZANGU.

1. Uchangamfu huondoa kinyongo – Hadhrat Rasuulullah SAW.
2. Bashasha huleta upendo – Hadhrat Seyidna Alli ra.
3. Pelekeaneni zawadi ili mpendane – Hadhrat Rasuulullah SAW
4. Upendo kwa wote pasi na chuki kwa yeyote – Hadhrat Mirza Nasir Ahmad

BAADHI YA KHULKA CHANYA ZA MUME KUISHAMIRISHA NDOA YAKE

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. ya kwamba mjumbe wa Allah SAW alisema: "Mkamilifu zaidi wa imani miongoni mwa waaminio ndiye aliye na khulka njema zaidi kuliko wengine. Na mbora wenu ndiye awatendeaye vizuri wakeze".

• Ewe mume, kuwa ni mwenye shukrani kwa mke wako. Onyesha shukrani njema.
• Mume umsifie mkeo kwamba leo mke wangu umependeza.
• Mume usifie chakula alichopika mkeo.
• Mume ujiepushe na kutoa simulizi au malalamiko ya ndani ya mji wako na kuanza kuhadithia ndugu mbalimbali katika hali ya kuomba ushauri wakiwemo marafiki. Kumbuka ndoa ilisimamiwa na washenga na mawalii, hawa daima ndio wawe ni washauri wako.
• Mume ujiepushe kumkaripia mkeo hadharani. Hayupo mke apendaye akaripiwe mbele za watu au mbele za watoto, kiustaarabu haipendezi na haifai kabisa.
• Siku moja moja basi mume uongozane na mkeo hata kwenda gengeni tu na umsaidie mkeo kubeba kikapu. Ufikapo gengeni, basi jaribu hata kuchagua fungu lililozuri la nyanya. Jambo hilo halitafutika na litabaki kwenye kumbukumbu za ndoa yenu.
• Mume jitahidi uongozane na mkeo kwenda masjid au kwenye jambo lolote lililoandaliwa kwa kushirikisha jinsia zote, basi mume uwe na mkeo pembeni.
• Mume uwe na desturi ya kusoma Qur'an uwapo nyumbani, na usome mbele ya mkeo. Athari hiyo njema itabaki kwa mke hata pale itokeapo siku mmepishana maneno ndani, basi mke akiifikiria hali hiyo hujirudi haraka na huomba maghofira kwa Allah.
• Mke aliye na utajiri, ni yule mwenye khofu na Allah nyakati zote.
• Mume ujijengee tabia ya kusali na mkeo uwapo nyumbani. Hii imebeba maana pana sana.
•Mume ujijengee desturi ya kumpelekea zawadi mkeo. Hata iwe ni zawadi ndogo mfano wa peremende, hakikisha unampelekea walau mara moja kwa mwezi.
• Mume uwe na khulka ya kumpa pole mkeo kwa majukumu yake ya nyumbani ya kutwa nzima.
• Mume ujiepushe na kutoa vitisho kwa mkeo pale akoseapo jambo, ujaribu kudhibiti ulimi na dhibiti hasira zako. Tunafundishwa kuwa ghadhabu zikikupanda sana, basi tawadha na umuelekee Allah.
• Mume punguza hali ya kupiga soga sana kwenye Whatsapp na mitandao ya kijamii hasa nyakati za usiku uwapo nyumbani. Jitahidi utoe nafasi kwa mke afurahie uwepo wako nyumbani, kwani kazi umeziacha huko mbali, sasa uwe ni muda wa familia tu.
• Mume utenge muda mzuri wa kuongea na familia, yaani jishushe kabisa na uwe huru kuongea na mkeo jambo lolote.
• Mume jitahidi sana kuonyesha hali ya kumheshimu na kumpenda mkeo.
• Unaporejea nyumbani basi onyesha hali ya bashasha usoni mwako.
• Mke akikosea kupika, usimfokee na ikibidi siku hiyo usiongelee jambo hilo. Tafuta siku nyingine ndio umwambie, tena ongea nae kwa upole.
• Mtumie mkeo ujumbe wa 'nakupenda sana mke wangu'

Lakini yatupasa sana kuikumbuka Hadithi hii isemayo: Mwanamke ni kama mfupa wa ubavu. Ukimnyoosha utamvunja. Na ukitaka kufaidika naye, basi faidika naye ilhali amepindamana. (Bukhari)

BAADHI YA KHULKA CHANYA ZA MKE KUISHAMIRISHA NDOA YAKE.

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. ya kwamba Mtume SAW alisema: Lau kama ningemwamuru yeyote kumsujudia yeyote mwingine, ningemwamuru mke kwamba amsujudie mumewe. (Tirmidhi)

• Mke punguza maneno maneno mengi kwa mumeo, maneno mengi huleta kero kwa waume.
• Mke onyesha adabu na utii wa dhati kwa mumeo, huyo ndio kiongozi wako.
• Mke epuka kuonyesha chembe zozote zile za kibri, kwa namna yoyote ile jiepushe.
• Mke kuwa mwepesi wa kuomba radhi pale ukoseapo, jishushe kwa mumeo hata kama upo sahihi.

Endelea uk 9

Kuepusha Migogoro na kujenga Mahaba katika Ndoa

Kutoka uk. 8

• Itokeapo kuna mzozo baina yako na mumeo, ishike njia ya kukaa kimya. Mtume s.a.w. alisema kuwa aliyefaulu ni yule aliyekaa kimya.

• Ewe mke, jaribu kubadilisha mfumo wa mpangilio wa ndani kwako mara kwa mara hususan sebuleni na chumbani kwako. Hali hii ya kubadilisha mipangilio huongeza ladha na hamu ya mumeo kufurahia mji wake hususan awe na hamu muda wote wa kuwepo nyumbani.

• Siku ukijua mumeo leo anapumzika, basi andaa chakula kizuri na akipendacho ili afurahie.

• Hakikisha mke unadhibiti hali zote za chumbani zisitoke, tunza heshima na siri za mumeo.

• Ewe mke uliyeolewa na mtumishi wa Allah na Jamaat, naomba uwe mwepesi kumsamehe mumeo ambaye muda mwingi hayupo nawe akimtumikia Allah. Msamehe.

• Mke usipunguze baadhi ya huduma na maandalizi ambayo awali ulikuwa ukimfanyia mumeo, lakini baada ya kuzoeana basi ukapunguza. Usikose katika hilo, utapalilia yasiyokuwepo.

• Mke ujifunze adabu njema za mwanamke wa Kiislam atakiwavyo kuwa, anza na mavazi.

• Mke punguza matamanio ya vitu nyumbani kwako na ikafikia hali ya kujifananisha na mama fulani au mke wa fulani. Ridhika na hali mliyonayo ili mdumu na mfurahie maisha ya ndoa.

• Mke jiepushe kabisa na makundi ya mashoga, wanaokuweka busy nyakati zote. Uzoefu unaonyesha kuwa pale unapoharibikiwa, marafiki na mashoga zako hukukwepa ili wasionekane wao ndio chanzo cha kukupotosha. Kumbukeni kuwa, sisi wanaume wengi ambao ni waaminio hatupendi hali zinazopitiliza za mashoga zenu.

• Mke uwapo nyumbani na mumeo, tafadhali dhibiti ulimi wako kwa vineno vineno yaani vijembe kumtupia mume. Baadhi ya vijembe vinakera, havipendezi kuvisikia. Jiepushe navyo.

• Muda wa sala unapowadia, jitahidi uwe wa kwanza kumkumbusha mumeo juu ya sala. Moja ya matendo ambayo huwa yanatufanya sisi waume zenu kutulia, ni khofu ya kuona huyu mke wangu anasali na anaomba, hebu nitulie nisije leta balaa.

• Mara moja moja jitahidi uamke kusali Tahajjud, tena siku ukiamka usiache kumuamsha na mumeo. Asipoamka na akashuhudia wewe unasali, hali hiyo huwa haitoweki kwa mwanaume na humjengea kuwa huyu mke niliyemuoa anayo khofu ya Allah, nidumu nae. Naye ataanza kutekeleza ibada.

• Mke ujidhibiti kunyanyua mguu wako na kwenda kwa rafiki yako, yaani kwa shoga yako.

• Jijengee mazingira ya kumuuliza mumeo anapendelea kula nini leo.

• Jiepushe kuonyesha ufahari na umaridadi wa nyumbani kwa wazazi wako na ukamuonyeshea mumeo, au ukaringia kwenu ya kwamba hakuna shida na mume asikusumbue. Hiyo ni sumu kwenye ndoa.

• Ikaribiapo mida yake kurejea nyumbani, muulize mumeo kwa maneno mazuri kuwa yupo wapi.

•Kuwa makini na matumizi mabaya ya simu na viujumbe tata kukufikia.

•Jiepushe na hali yoyote ile ya kumdharau mumeo kwa hali yoyote ile aliyokuwa nayo, iwe ni uduni wa kazi au uduni wa makazi, usimdharau.

•Mke aliye na utajiri, ni yule mwenye khofu na Allah nyakati zote.

•Hata ipitapo miaka 10 ya ndoa yenu, onyesha kwa mumeo hali ya upendo na kumthamini.

•Itokeapo siku ukabana matumizi kutoka kwenye bajeti yako, basi mnunulie mumeo hata msuli tu au malapa. Hali hiyo itahuisha udhia uliokuwepo na kuleta upendo.

•Ewe mke, punguza sana kumuhadithia mama yako mzazi mambo ya mumeo na mnavyoishi.

•Mke mwema ni yule anayeonyesha na atoae shukrani njema kwa mumewe kwa jambo lolote.

•Mke ujitahidi kusoma Qur'an ukiwa peke yako na ukiwa na mumeo, msomee mumeo Qur'an.

•Mke shirikiana na mumeo katika kumkumbusha ibada mbalimbali na matendo mema ikiwemo kujiandaa hata kwa ibada ya hijja mjaaliwapo uwezo na uhai basi muitekeleze pamoja.

•Iwapo mumeo atakukosea, basi mlipe wema maradufu na ujishushe sana.

•Ewe mke mnapokwama kiuchumi, basi mshauri na kuwa karibu mno na mumeo. Mpe ushauri.

•Wanunulie wifi zako zawadi na uwapelekee, wapelekee zawadi wazazi wa mumeo.

•Mke onyesha ukarimu mwema pale wageni wawatembeleapo, mjaaliwapo basi watayarishie chakula kizuri na nyumba ipambe.

•Mke jiepushe ukaribu na marafiki wa mumeo, wala usiwahadithie hali yoyote ya ndani mwenu.

•Mke ujijengee mazingira ya kuwapigia simu wazazi wa mumeo na kuwasalimu.

•Iwapo mumeo hayupo, basi jitahidi sana uwe mwema kwa wageni au wazazi au ndugu wa mumeo wajapo kuwatembelea.

•Usitoke nje ya nyumba yako bila ruksa ya mumeo, jilinde kwa mavazi yenye stara.

Nikiwa nahitimisha uwasilishaji wa mada yangu hii, napenda niwape mfano mmoja ambao Hadhrat Khalifatul Masih 5th (atba) alimpatia tena ndugu Abid Khan. Siku moja Hudhuur alikuwa ofisini kwake pale Masjid Fazl, London. Akiwa ofisini, alimuona ndugu Abid Khan akiingia maeneo ya Masjid Fazl huku akiwa ameongozana na mkewe. Baadae Hudhuur alimuita ndugu Abid Khan ofisini na kumwambia kwamba, nimekuona ukiingia maeneo haya ukiwa umefatana na mkeo. Nimeona wewe ukiwa mbele na mkeo akiwa nyuma yako. Abid Khan akasema naam, ni kweli Hudhuur. Pale Hudhuur akamshauri kuwa, unapokuwa upo na mkeo mnatembea, hakikisha mkitembea sambamba, wewe usiwe mbele wala yeye asiwe nyuma. Mfano huu ulio hai alioutoa Hadhrat Khalifatul Masih tunajionea jinsi unavyodumisha ndoa zetu na ulimuondolea ndugu huyo kutoka katika udhia wa kutozingatia baadhi ya vitu vidogo vidogo vipelekeavyo athari, kwamba ndoa ni kioo kwetu na jamii nzima zinazotutazama. Na kikubwa zaidi kwetu sisi wanandoa, tudumu na tuimarishe mapenzi na urafiki wetu na Khalifa wa zama, kwamba hali zetu tuwapo katika sintofahamu basi tuombe msaada wa ushauri kutoka kwake pia tujikite zaidi kwenye matendo mema na taqwa. Namuomba Allah mtukufu mwenye enzi, Atujaalie semina hii kwetu wanandoa basi ituhuishe sote, ihuishe nyumba zetu, ihuishe upendo baina ya mke na mume leo, kesho mpaka mwisho wa hatma zetu hapa duniani Insha'Allah.

Waakhiru da'awana,

Walhamdulillah rabbil alameen.

Safari Ya Umrah

Kutoka uk. 12

kama anapanda juu.

Muda huu, kila mmoja hua kivyake.. mwili na moyo pia hujihisi ubaridi wa kipekee, huku akiendelea kumtukuza Allah.. kwa kuitikia wito wa Mola wake kwa Sauti ya chini kwa maneno haya:-

Labbeik allaahumma labbeik, labbeik laashiriika laka labbeik. Innal hamdah, wanni'mat... laka wal'mulk laashiriika laka

Yaani... *Nipo hapa Eee Mola wetu nipo hapa.. Nipo hapa eewe usie na mshirika nipo hapa.. Hakika sifa zote njema, Neema zako na Ufalme wako.. huna mshirika*

kwa maneno haya ya utii, hujjaji huendelea kutukuza hivi muda wote mpaka kuifikia nyumba ya Allah mpendwa..

Kuingia Masjid Haraam

Baada ya kuwasili Makkah, mahujjaji huelekea moja kwa moja Masjid Haraam.

Msikiti huu mkubwa, wenye heshima na utukufu kabisa upo katika umbile ambalo la kipekee. Hujjaji anaweza kuingia moja kwa moja kutoka mahala popote anapotokea, kwa maana msikiti huu una milango pande zote.

Kwa sasa jumla ya Milango 37 inaingia katika msikiti huu kuwawezesha Mahujaji kuingia kutoka Pande zote, na inaweza kuongezeka kwa kuwa



Barabara kutoka Miqaat kuelekea Makkah

marekebisho bado yanaendelea kufanyika ili kukidhi mahitaji.

Kati ya Milango hiyo 37.. ambapo lango Namba 1 ni ***King Abdul Aziz Gate.***

2. Kuzunguka Kaaba (Tawaf)

Pamoja na Ukarabati na maboresho yanayoendelea kufanyika katika msikiti huu wa Makkah, lakini bado kuna njia elekezi zitakazo kuelekeza hujjaji ni vipi utaingia na kuanza kufanya ibada yako.

Pia kuna Askari waangalizi wa msikiti na wahudumu wengine ambao hutoa maelekezo kwa mahujjaji ikiwemo mabango elekezi kwa wanaoweza kusoma yaliyo katika Ghorofa au tabaka ya chini ya Masjid Haram eneo kunafanywa Ukarabati na maboresho katika kisima cha Maji (Zam zam).

Pia kuna vijarinda ambavyo vinapatikana ile sehemu ya maandalizi Miqaat, pia vikitoa maelekezo.

Lakini pamoja na hayo, ni muhimu pia hujjaji wa Umrah na Haji kupata elimu ya msingi kuhusu Haji nyumbani kabla ya kufanya safari, maana mtu akishakuwa kule, si rahisi kuyakumbuka yote kwa muda mfupi.

Jinsi ya kuzunguka Kaaba

Katika Lugha ya Alama, Kuzunguka kitu, humaanisha kukipenda na kuwa tayari kukilinda, japo kuna maana na falsafa Pana juu ya Ibada nzima ya Haji.. lakini lengo ni kuamini juu ya Mungu mmoja, kuabudu katika hiyo, na kutangaza Umoja wa Mungu.

Baada ya kuingia Baitullaahil haraam hujjaji huanza moja kwa moja kuizunguka Kaaba.

Mzunguko wa Kaaba unatofautiana kulingana na hujaji anazunguka akiwa umbali kiasi gani na Kaaba, Yule aliye karibu zaid huwa na mzunguko mfupi ukilinganisha na Yule aliye mbali hasa wale wanaozunguka mzunguko wa Ghorofani.

Pamoja na yote mizunguko yote huanzia sehemu moja mahala lilipo Jiwe jeusi

hivyo wale waliombali kuna alama ya Taa ya Kijani kuonyesha mzunguko unapoanzia, hesabu ya mzunguko mmoja huhesabika kila unapolifikia Jiwe jeusi kwa walio karibu na Kaaba, na Alama ya Taa ya Kijani kwa wenye mizunguko iliyo mbali na Kaaba.

Haijalishi hujaji atatumia Muda gani, kwani ibada Ile ya kuzunguka haiongozwi na Imamu kama zilivyo sala zingine, na vile Hujaji atakavyojisikia moyo wake unatosheka, kwa kumtukuza bwana Mungu wake Mpendwa, kwa kujinyenyekeza na kuonyesha upendo kwake.

Hujaj ataendelea kuitikia maneno ya wito wa Mola wake, *Labbeik allaahumma labbeik... labbeik laasharika lala labbeik...*

Pia kuzidisha kumtukuza Allah kwa tasbihi na dhikri nyingi moyoni kadri uwezavyo..

Maneno kama *Sub'haanallaahi wabihamdihi, sub'haanallaahil adhiim*

Yaani; Umetakasika ee Mola wetu kwa sifa njema, Umetakasika ewe Mola Mwenye heshima kuu

Na zingine nyingi zenye kumtukuza Allah hapa ndo mahala pake.

Katika kuzunguka, hujaji atazunguka huku Kaaba ikiwa upande wake wa kushoto, na kila mara anapomaliza mzunguko mmoja kwa kulifikia jiwe au usawa wake, atainua kidogo mkono wake wa kuume kwa kuwa yupo mbali na kutamka maneno haya..

Rabbaanaa aatinaa fiddun'ia hasanah, wafil aakhirat hasanah waqinaa adhaaban naar,

Yaani: Ee Mola wetu Utupe mambo Mema katika dunia, na Utupe mambo mema katika Akhera, na Utukinge na adhabu ya Moto.

Ni vizuri kuwa mwangalifu katika dhikri na Tasbih kwa Allah kwa kutumia maneno ya Maana yaliyo katika Quran tukufu, na dua za Mtume s.a.w. hata kama yatakuwa mawili au matatu, na kuyarudia hayo kwa kukariri ukiwa na yakini, badala ya kutamka maneno mengi yasiyokuwa na maana au kutojua unachoomba.

Hujaji atazunguka Kaaba mara 7 huku akianza na mizunguko minne ya mwanzo kwa mwendo wa taratibu, na kumalizia mitatu ya mwisho kwa kuongeza kidogo kasi ya mwendo kama mazingira yanaruhusu (yaani kama hakuna msongamano mkubwa).

Itaendelea toleo Lijalo

Safari Hiyo!

Kutoka toleo Lililopita

1. Miaka ya 1960 tulikuwa na jarida lililokuwa linatolewa kila mwisho wa mwezi, lililoitwa 'Habari za Ahmadiyya'. Jarida hili lilikuwa ni kwa Waahmadiyya tu. Humo zilikuwa zikitoka habari za hotuba za Khalifa Mtukufu, harakati za mahubiri na matukio mengine mengi yanayohusu Wanajamaat kama vifo, ndoa na kuzaliwa watoto. Jarida hili lilikuwa linachapishwa hapa hapa Makao Makuu Masjid Salaam. Kwa hakika jarida hili lilifanya kazi nzuri ya kuhifadhi historia yetu. Baadhi ya wahariri wa jarida hili walikuwa ni Mwalimu Hamisi Wamwera na Bw. Ramadhani Abdallah Marunda. Mzigo wa kuchapisha jarida hili aliubeba Ramadhani Athumani Shamte ambaye alilitendea haki jarida hili kwa kuhakikisha kwamba lilikuwa likitoka kila ifikapo mwisho wa mwezi bila kukosa. Bw. Shamte alikuwa tayari kuacha kazi zozote zile mpaka ahakikishe Habari za Ahmadiyya limetoka.

2. Ukitaka kazi ifanyike kwa usahihi na kwa muda, basi kazi hiyo mpatie Bw. Ramadhani Athumani Shamte bilkhususi kazi hiyo ikiwa ya dini. Hayo ndiyo yalikuwa maoni ya maulana Sheikh Jamil Rahman Rafique ambaye amewahi kuitumikia Jumuiyya ya Ahmadiyya katika Afrika Mashariki akiwa Amir na Mbashiri Mkuu Kenya na Tanzania. Wakati yupo nchini Sheikh Jamil Rahman Rafique Jalsa moja ilifanyika mjini Tabora mahali paitwapo Ibili. Ilibidi Jamaat ikodi behewa la Treni kuwabeba Wanajamaat kutoka Dar es salaam hadi Tabora. Kazi hiyo ilisimamiwa na watu watatu (3), Marehemu Mzee Mussa Kiziara, Mohammed Saidi Kibindu na Ramadhani Athumani Shamte. Akiwa amevalia mavazi yake ya mgambo Shamte alitupanga vizuri kwenye behewa letu na safari yetu ilikuwa ya salama na tukafika salama salmini. Enzi hizo Jalsa Salana ilikuwa inazunguka kutoka mkoa mmoja hadi mwingine. Yalipatikana matatizo madogomadogo kwa mathalani huko Ibiri tulipata tatizo kubwa la maji, Sheikh Jamil Rahman Rafique aliongoza maombi na Alhamdulillah mvua iliweza kunyesha. Tukafaidika sote tuliokuwa kwenye mkutano na wakafaidika pia wenyeji wa kijiji hicho. Katika mkutano huo ulinzi ulikuwa mkali na Bw. Ramadhani Shamte ndiye aliyekuwa Mkuu wa kikosi cha Ulinzi.

3. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa daktari wa vitabu vikuukuu, alikuwa anavikusanya na kuviweka pamoja katika sura ya kitabu (binding) yakiwemo pia na magazeti ya Mapenzi ya Mungu. Wanajamaat wengi walitumia ujuzi wake kuhuisha vitabu vyao. Kazi hii aliifanya kwa furaha kubwa. Na Bw. Shamte akikuambia; kazi yako Inshallah itakamilika tarehe kadhaa na siku kadhaa basi uamini ya kwamba kazi yako utaipata siku hiyo hiyo.

4. Ramadhani Athumani Shamte aliipenda sana Jamaat. Kila nilipokwenda kwake kumjulia hali kutokana na maradhi yake, mara kwa mara alikuwa akiniuliza juu ya maendeleo ya Jamaat. Na katika Jalsa Salana ya mwaka uliopita alitamani sana kuhudhuria, lakini ni udhaifu wa mwili ndio haukumruhusu.

Ulimwengu wa Kiswahili umempoteza mshairi mahiri. Mtulivu katika tungo zake, makini katika uteuzi wa maneno, bingwa katika fani, papara ilikuwa bidhaa mbovu hakuinunua. Ni msimamo wake huu ulionifanya niomboleze;

1 Mashairi ya kuchoma, utadhania mshale
Na ya kuondoa homa, kwa wale walo na ndwele
Mashairi ya hekima, na elimu vile vile
Kwa kifo chake Shamte, dhahiri yatapungua.
2 Mashairi ya adabu, bila tusi na kelele
Mashairi ya wajibu, unasi tutumikile
Mashairi ya kutibu, watoto hata wavele
Kwa kifo chake Shamte, kisima kimekauka.
3 Mashairi yenye vina, muwala ukiwa tele
Mizani ilo lingana, ya huyu mzungupule
Imeshazama safina, bidhaa zitokomele
Kwa kifo chake Shamte, duka nalo tumefunga.

BURIANI RAMADHANI ATHUMANI SHAMTE (AKILI SI MALI)

Kwa masikitiko makubwa, tumepata habari za kutawafu kwa ndugu yetu, mpenzi mkubwa wa Jumuiyya ya Ahmadiyya, shujaa ambaye hakuwa na woga akitumwa kuitumikia Ahmadiyya, mshairi aliyeitumia kalamu kuwaamsha waliolala na kuwaambia ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa amekwishafika. Mtaalamu aliyetumia kipaji chake cha uchapaji kuchapa mambo ya kheri na manufaa. Bwana aliyejikusanyia sifa zote hizi ni Bw. Ramadhani Athumani Shamte (Akili Si Mali) ambaye tulitengana nae kimwili tarehe 04/03/2018 na kuzikwa kwenye makaburi yetu Wailes Temeke na umati wa waombolezaji. Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Bw. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa na mapenzi ya dhati na Jumuiyya ya Ahmadiyya, leta utani na masikhara lakini sio katika mambo yanahusu Jamaat, mtakosana mpaka ujirekebishe. Mapenzi yake yalimpelekea hadi kutafuta gazeti lolote au kitabu kilichoigusa Jamaat kwa ubaya, huko atakinunua kwa pesa yake na atakileta Msikitini na kumuomba Sheikh ampe dawa Mwandishi wa upotoshaji huo. Lakini alipoweza yeye hakusubiri. Hakuchelewa, alishika kalamu na kutoa jibu lililotuacha sote tumetulia na kuridhika. Sifa hii alikuwa nayo Bw. Shamte. Sifa hii inatakiwa sasa zaidi kuliko wakati uliopita. Magazeti yamekuwa lukuki, vitabu vingi vimetungwa, mitandao ndio usiseme, panahitajika Wanajamaat wanaopita hukuna huko wakitafuta mtu yeyote anayeigusa Jamaat na hapo hapo anaoneshwa njia iliyonyooka.

Bw. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa Mshairi. Alipendwa na kuheshimiwa na wengi. Hakukosa kwenye mikutano ya Washairi na huko kwenye redio ya taifa alikwenda mara kwa mara. Lakini katika harakati zake za ushairi yeye alitanguliza Jamaat Ahmadiyya. Alihubiri Ahmadiyya. Alifafanua mafundisho ya Islam kama yanavyofafanuliwa na Ahmadiyya. Kwake sanaa hii ya ushairi ilikuwa ni silaha ya mahubiri. Silaha muhimu ya kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Kuna somo kubwa kwa sisi tuliyobaki kujitahidi kutumia vipaji tulivyopewa na Allah kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Sote Allah Ametupatia vipaji mbalimbali. Tujiulize! Ni kwa kiasi gani kipaji nilichopewa mimi kinatumika katika kupeleka mbele ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa? Swali hili alilijibu kwa vitendo Bw. Ramadhani Athumani Shamte. Nasi tukumbuke kufanya hivyo. Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo.

Kabla ya maradhi Bw. Ramadhani Athumani Shamte kama unavyomuona samaki baharini basi naye bahari yake ilikuwa Masjid Salaam. Hakukosa asilani. Akitoka nyumbani kwake Kinondoni Moscow kwenye baiskeli yake kituo chake cha kwanza ni Masjid Salaam. Ataweka baiskeli yake na amuulize Sheikh kama kulikuwa na kazi yoyote apewe. Na akipewa ataifanya kwa bidii. Akitoka kazini atapita tena Masjid Salaam na kuhudhuria darasa lililokuwa linaendeshwa na Maulana Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry. Shughuli zote hizo zikiisha ndipo anaanza kufikiria kurudi nyumbani. Na pengine mazungumzo yangemkamata hadi saa tatu usiku. Mahali alipokuwa Hemedi Feruzi Mahmood Mbayana, Athumani Mlandura, Mohammedi Kibindu, ilikuwa ni vigumu kutoka. Kwa ujumla Shamte alikuwa samaki na Masjid Salaam bahari yake. Tunao wajibu nasi wa kugeuza Masjid Salaam tena sasa Masjid Salaam mpya iwe bahari ili tupate shabaha ya kuumbwa kwetu ambako ni kumuabudu Allah.

Tunaungana na Al-Ustadhi Abdallah Hamis (Kungwi) katika kuomboleza;

Kwetu alikuwa pete, pambo lenye unadhifu
Twamuombea apate, pepo ya Mola Raufu
Baraka zimuambate, apewe hadhi tukufu.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

… Msiogope laana ya dunia, kwani inapotea mara moja kama moshi, wala haiwezi kubadilisha mchana uwe usiku. Bali ogopeni laana ya Mungu inayoteremka mbinguni na kuangamiza kila inayemteremkia katika dunia na akhera.

… Fanyeni suluhu upesi ninyi kwa ninyi na sameheni makosa ya ndugu zenu kwani ni mtu wa shari asiyekuwa radhi kufanya suluhu na ndugu yake, yeye atakatwa kwa sababu ya kuachanisha watu.

... Mkitaka Mwenyezi Mungu awe radhi juu yenu mbinguni basi kuweni kama ndugu wawili waliozaliwa katika tumbo moja. Mbora wenu ni yule mwenye kusamehe sana makosa ya nduguze.

Safina Ya Nuhu

MANENO YA BUSARA

Ukiiona kasoro au aibu yoyote kwangu, basi niambie mimi mwenyewe,
Wala usimwambie mtu mwingine yoyote, Mimi mwenywe ndie mwenye haki zaidi ya kubadilisha aibu yangu.
Ukiniambia mwenyewe, itakua ni nasaha na utapata ujira wako kwa Allaah.
Na ukimwambia mwingine utakua umenisengenya na ni dhambi.
Kwanini inakua watu wakiona aibu au kosa kwa mtu, wanawatangazia watu wote wa mbali, wakati mwenye kasoro hiyo mwenyewe hawamuambii??
Watu wengi wana uhodari wa kutangaza mambo ya watu hata kama hawana ushahidi juu ya hayo,, lakini ufundi wa kuwaambia wenyewe hawana.
Nilifurahishwa na maneno ya moja kati hoteli niliyowahi kutembelea:
Nimefurahishwa sana na ibara niliyoiona imeandikwa katika hotel ile:
"*Ikiwa tumekuridhisha kwa huduma zetu, basi wewe sema kwa watu, na kama hatukukuridhisha basi tuambie wenyewe*"
Hebu tuifanyie kazi ibara kama hiyo, itakua suala la kusengenya halipo tena. Maisha haya ni sawa na historia fupi sana, nayo ni:
Tumetoka katika udongo, tukaishi katika udongo, kisha tunarudi katika udongo, kisha hesabu, imma thawabu na immaa iqaabu- yaani adhabu.
Ikiwa umeona au kusikia jema la watu basi litangaze lau utaona udhaifu au pungufu la kibinaadamu basi sitiri nawe utasitiriwa.
Basi ishi maisha yako kwa ajili ya Allah, utakua ni mbora wa viumbe vya Allah.

MAPENZI YA MASIHI ALIYEAHIDIWA (AS) KWA QUR'AN TUKUFU

Hotuba iliyotolewa na Sir Maulana Ifikhar Ahmad Ayaz kwenye Jalsa Salana ya Tanzania mwaka 1977/78

Sir Iftikhar Ayaz aliletwa nchini Tanzania na aliitumikia Idara ya Elimu na baadaye aliitumikia CIRDAFRICA, Jumuiya ya Madola, Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa na UNESCO. Alianzisha Shirika la Jumuiya ya Madola nchini Tanzania na akawatumikia Watanzania katika nyanja mbalimbali. Sasa anatumikia ubinadamu kama Balozi wa Amani na Mwenyekiti wa Kamati ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Amezuru sehemu mbalimbali za ulimwengu akihutubia mikutano ya amani na kufikisha ujumbe wa kweli wa Uislam. Sir Iftikhar pia alipata baraka ya kuanzisha Jamaat Ahmadiyya huko Tuvalu na visiwa vingi vya Pasifiki. Pia ametumikia Jamaat nchini Uingereza kama Sadr Ansarullah na Amir wa Uingereza. Amepokea tuzo zaidi ya arobaini kutoka nchi tofauti na mashirika ya dunia. Hivi karibuni, alichaguliwa Kamanda wa Knight wa Dola ya Uingereza kwa cheo cha 'Sir'.

Upo ushahidi wa kutosha kuhusu maisha yake kutoka kwa wale waliomuona katika maisha yake ya mwanzo, halikadhalika kwa wale aliosuhubiana nao utotoni. Wao hushuhudia kuwa hata wakati wa ujana wake, wakati ambapo vijana hujishughulisha na papara papara za michezo ya kitoto, Hadhrat Ahmad (as) alijishughulisha katika kusoma Qur'an Tukufu na kumtafakari Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo alivyoutumia muda wake. Ushahidi huu umepatikana kutoka kwa ndugu, marafiki, na halikadhalika kutokana na wale wahusianao nasi.

Hadhrat Khan Bahadur Mirza Sultan Ahmad alikuwa mwana wa Hadhrat Ahmad (as) kwa mkewe wa kwanza. Yeye hakujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya katika uhai wa baba yake. Alijiunga na Jumuiyya mkononi mwa Hadhrat Al-Musleh Maood – Khalifa wa pili. Hadhrat Mirza Sultani Ahmad aliandika yafuatayo kuhusu maisha ya awali ya baba yake; "Yeye (yaani Hadhrat Ahmad as) alikuwa na makala moja ya Qur'an Tukufu na ambayo aliipigia mistari kila alipoisoma bila ya kutia chumvi naweza kusema bila hofu kuwa aliweza kuisoma Qur'an Tukufu zaidi ya mara elfu kumi" (Hayaatal Nabi Uk.108)

Na sasa tuchunguze ushuhuda wa mtu ambaye hakuwa ndugu yake. Wakati huo Hadhrat Ahmad (as) alikuwa akifanya kazi ya serikali huko Sialkot. Alikubali kufanya kazi hiyo kwa kumtii na kumridhisha baba yake aliyemuamuru kufanya hivyo. Matashi yake yanadhihirika katika mojawapo ya mashairi yake lisemalo; Dola na milki zinanifalia nini mimi, kwani kazi yangu na wito wangu ni tofauti sana. Zanihusu nini mimi taji za kifalme kwani taji yangu ni furaha ya mpendwa wangu, (yaani Mwenyezi Mungu). Mfuasi wake mmoja, Hadhrat Sheikh Yakubuh Ali Irfani alisema; Ilikuwa tabia yake Hadhrat Ahmad (as) kwamba kila alipokuwa chumbani mwake alifunga mlango. Alifanya hivyo pia alipokuwa Sialkot. Ni mara chache sana alikwenda kuwatembelea watu. Baada ya kumaliza kazi zake mahakamani, alirudi chumbani kwake kuketi mlango ukiwa umefungwa. Hapo alimgeukia Mwenyezi Mungu na kumtafakari. Baadhi ya waduku zi walipotaka kujua anafanya nini walimfuatafuata na kumnyemelea alipofunga mlango ili wadadisi. Hapo walifaulu kujua kile alichokuwa akifanya Hadhrat Ahmad (as) walimuona ameketi katika mswala, akishikilia Qur'an akiomba Dua kwa makini, akisema; "Ee Mola wangu hili ni neno lako, unijaalie ili nilielewe vyema, alidumu kuomba hivyo ndani ya maandiko, mazungumzo na katika hotuba zake.


Dr. Iftikhar Ahmad Ayaz

Kwa kawaida wazungumzaji wengi na waandishi wana tabia ya kusoma vitabu na maandishi mbalimbali kabla ya kuanza kusema au kuandika. Lakini kama vile mfuasi wake Hadhrat Ahmad (as), Hadhrat Mufti Mohammad Sadiq alivyosema, Hadhrat Masihi Maood alisoma Qur'an Tukufu wakati wote. Ni mara chache tu alisoma maandiko mengine. Kwa ujumla maandishi yake yote ni ufafanuzi wa maandishi ya Qur'an Tukufu. Halikadhalika tenzi zake. Katika tenzi moja ya urdu, Hadhrat Ahmad (as) anasema; "Ee Mungu wangu, ni mkusanyiko gani huu katika kitabu chako Qur'an Tukufu? Kitabu hiki ni chem Chem ya elimu na maarifa yote ya maana kwa binadamu. (Shumaael-i-Ahmad uk.24)

Hadhrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad Sahib aliandika hivi; 'katika silsila Ahmadiyya'; "Mtu mmoja aliyemuona Hadhrat Ahmad (as) akiwa katika gari la farasi akitoka Qadian kwenda Batala alieleza kuwa mara tu baada ya kutoka Qadian, Hadhrat Masihi Maood alikifungua kitabu cha Qur'an Tukufu, hakufungua ukurasa mwingine kwa safari nzima ya umbali upatao saa 5. Aliutumia muda wote huu akizama katika ukurasa mmoja tu wa Sura Al-Fatiha.

Inawajibika kutoa dondoo moja kutokana na maandishi ya Hadhrat Ahmad (as), dondoo ionyeshayo jinsi sura hii ya Al-Fatiha ilivyo muhimu mno. Zaidi ya hayo itaonyesha ni kwa nini yeye aliipenda na alizama katika sura hii mara kwa mara. Hadhrat Ahmad (as) alisema; yale niliyoyaandika kuhusu uzuri wa Sura ya Al Fatiha ni jambo la dhati hasa na ambalo halina kifani. Iwapo mhakiki asiye na upendeleo ataichambua sura hii kwa makini, elimu na maarifa yake pamoja na mtindo wa uandishi na umahiri wa lugha, na iwapo atalizingatia kina cha maarifa yaliyomo humo, ambayo hububujika kama chem chem ya wema na iwapo atazingatia na kutafakari maana ya kiroho ambayo husafisha giza lililomo moyoni kwa namna ya pekee na kuifanya nuru ya mileleku wa baraka hakika atatambua utukufu wa kimbingu uliomo katika Qur'an Tukufu, ambayo hupita uwezo wa kibinadamu kuielewa. Hivyo mhakiki makini huyo ataweza kutambua ukweli ambao ubongo wa mwanadamu hauwezi kuutambua. (Baraheeni Ahmadiyya Sehemu ya 4 uk.544-545 ya dondoo).

Vilevile Masihi aliyeahidiwa (as) huandika katika "Ejaaz-al-Masih"; Sura ya Al Fatiha ni ngome imara, nuru halisi, mwalimu na nguzo muhimu ya Qur'an Tukufu. Halikadhalika huilinda Qur'an, moyo mweupe na mawazo kama mwako wa taa, na uelekevu halisi, ataitambua kuwa nuru na ufunguo wa siri zote. Zaidi ya yote umuhimu mkuu wa sura hii ni kwamba imeeleza sifa zote za Mwenyezi Mungu kwa jinsi ipitayo uwezo wa mwanadamu yeyote. (Uk.20-21)

Hadhrat Mufti Mohammed Sadiq rafiki wa Seyidna Ahmad (as) ameeleza; Nimemwona Seyidna Ahmad (as) mara moja tu akilia. Haya yalitokea wakati alipokwenda kutembea na rafiki zake. Wakati huo kijana mmoja mkwe yake Haji Habibur Rahman wa Pura alikuwa amekuja Qadian. Mtu mmoja alieleza kuwa kijana huyo aliweza sana kusoma Qur'an kwa ghaib. Papo hapo Hadhrat Ahmad (as) aliketi kando ya barabara na kumwomba afanye hivyo kwa kusoma sehemu ya Qur'an Tukufu. Kijana huyo alifanya hivyo. Hapo basi nikayaona machozi yakimtiririka. (Zikri-Habeel uk.323)

Ningependa kueleza kwa unyenyekevu kuwa machozi yalikuwa sehemu ya pendo yaliyobubujika moyoni mwake, na ambayo pia aliyaelezea katika moja wapo ya tenzi zake za urdu alisema; "Ninayo hamu kuu moyoni mwangu ya kukibusu milele kitabu chako na wakati wote kukishika kitabu hiki Qur'an kwani hiki pekee ndiyo kitabu". Bali ilikuwa muhimu sana kwake kuhakikisha kuwa binadamu wote huutambua umuhimu wa johari hiyo na kunufaishwa nayo. Ameielezea hamu hiyo katika beti chache za Kifarsia.

1. Maishani mwangu mwote ninateseka kwa ajili ya huzuni kuhusu kitabu hiki ambacho kimesababisha nikate tamaa ya maisha.
2. Ningeruka kwa shangwe mara mia kama ningesikia habari za kufurahisha na za kuvutia za Qur'an Tukufu zimezagaa na kukubaliwa ulimwenguni kote.
3. Ee rafiki mpenzi, tamasha za dunia hii ni za muda zaweza kudumu kwa juma moja hivi, kwani hakuna yeyote aliyebakia ulimwenguni milele.
4. Kama moyo wako haukuumi leo kwa ajili ya Qur'an Tukufu, ifikapo siku ya hukumu hutakuwa na msamaha kwa maovu yako mbele ya Hakimu wa pekee.

Hadhrat 'Masihi Maood' Masihi Aliyeahidiwa katika maandishi yake, katika majadiliano yake na makusanyo yake binafsi, licha ya kufafanua kwamba Qur'an Tukufu ni sheria ya wakati wote, alifafanua jinsi Qur'an Tukufu kilivyo kitabu kikuu na maarufu kuliko vitabu vingine vya maana katika dini mbalimbali. Halikadhalika amefafanua majanga yatakayoipata dunia pamoja na utatuzi wake, alieleza wazi faida ya kuyatii mafundisho yake. Hapa nitatoa dondoo chache tu. Seyidna Ahmad (as) anasema; "Kama mtu yeyote hukanusha nguvu za Qur'an Tukufu, tunachukua dhima ya kumthibitishia ukweli kwamba Qur'an Tukufu ndiyo ghala ya ukweli na mafundisho yote yaliyo halisi na matakatifu" (Malfoozat Jal. I Uk.84)

"Kama mtu yeyote atakuwa tayari kutuonyesha ubovu wa mafundisho ya Qur'an Tukufu hata kwa chembe moja ndogo sana alfu mara, au kama akiweza kuonyesha kwa kiasi hicho hicho jinsi mafundisho hayo yalivyo hafifu kulinganisha na mengine, tutakuwa radhi kufa" (Baraheen Ahmadiyya uk.268).

Hadhrat Ahmad (as) ametueleza yafuatayo baada ya kuashiriwa na Mwenyezi Mungu; "Ninakuhakikishia kwamba sikuona kitabu kingine cha dini, mafunzo ya dini, ikiwa ni katika kanuni muhimu za wema, ama sehemu mojawapo ya utimilizaji wa kazi za jamii, au matendo ya utakatifu ambacho kimetoa mafunzo kulingana na Qur'an Tukufu. Haya si maoni yangu binafsi na wala ushahidi huu niutoao hautoshelezi, bali natamka haya wakati ambapo ulimwengu umo katika malumbano ya dhana mbalimbali za dini nami nazungumza yale niliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu" (Paighan Sulh).

Seyidna Ahmad (as) pia aliandika hivi; "Mwenyezi Mungu Mtukufu alijua wazi kuwa elimu mpya ya sayansi itazuka, hata hivyo hakuna utafiti wowote au sayansi itakayoweza kufaulu kupingana na Qur'an Tukufu wala hakuna ukweli wowote uwezao kuwa bila ya kuwa na misingi yake katika Qur'an Tukufu". (Malfoozat Jal. I uk.400).

Itaendelea toleo Lijalo

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JUM II - RAJAB 1439 AH | MEI 2018 | AMMAN 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat 'Adil bin hatim r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Jikingeni na Moto walau kwa (kutoa katika njia ya Allah) kipande cha tende. (Bukhari)

Mtaalamu Aliyefasiri Qurani Tukufu Katika Kichina
Muhammad Usman Chuchingshi sahib

Baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Mtalaamu mmoja wa Jamaati bwana Uthman wa China amefariki katika siku za karibuni. Allah Alimwezesha kutoka katika maeneo ya mbali Zaidi ya China na kuja Pakistani kisha kujiunga na Jamaati. Yeye alijitolea maisha yake kuwa waqfu naye aliweza kuandika mwenyewe juu ya maisha yake na mambo haya ni mapana na marefu zaidi, yenye kuongeza imani nami siwezi kuyaeleza yote. Kuna muswada unaofaa kwa ajili ya kuandika kitabu kizima kuhusu maisha yake na Majlis Khuddamul Ahmadiyya Pakistan inaweza kulitekeleza vizuri jukumu hili. Ningependa kueleza mbele yenu baadhi ya kumbukumbu ya mtawa huyu ambaye ni mfano wa kuigwa kwa ajili ya kila Muahmadiyya na Waqfiin pia.

Jina lake lilikuwa Muhammad Uthman Chuchingshi, alizaliwa mnamo 13-12-1925 na kufariki 13-04-2018. Alijifunzia masomo kadhaa pamoja na siasa, sheria, falsafa na dini. Alijiunga na Jumuiyya mnamo 1949 baada ya kufanya utafiti. Alijitolea maisha yake kuwa waqfu mnamo 16-08-1959 na kujiunga na chuo cha Jamia Ahmadiyya Rabwah Pakistan na kuhitimu mnamo 1964 na kujipatia cheti cha shahada. Aliitumikia Jumuiyya katika idara ya Tasniif Rabwah na katika mji wa Karachi Pakistan kisha katika nchi za Singapur na Malaysia na kurudi Pakistan mnamo 1970. Alibahatika kuenda kufanya Hijja Na Umra (ziara ya Kaaba). Aliitwa Uingereza baada kuanzishwa kwa kazi ya dawati la Kichina na aliweza kuandika vitabu 7 vya kwake na kutafsiri vitabu 35, ikiwemo tafsiri ya Qur'ani Tukufu katika



Bwana Muhammad Uthman Chuchingshi wa China enzi za uhai wake

Kichina, iliyokamilika katika muda wa miaka minne. Tasiri hii ilichapishwa na Jamaat na ina sifa zake za pekee zilizoelezwa na wanazuoni kadhaa wa Kichina, kuna profesa wa Kichina aliyeandika maoni yake juu ya tafsiri hii kwa kurasa 15 na alisema kwamba bwana Athmani anatoa kumbukumbu zinazounga mkono na tafsiri yake na tafsiri yake inaeleweka vizuri zaidi kuliko tafsiri za watu wengine ambazo hazifahamiki vyema.

Huzur atba alisema bwana Uthman alikuwa mtu wa kawaida, mwenye kufuata maamrisho yote ya dini na kufunga sana saumu na kuelewa kuwa Qur'ani Tukufu ni kitabu kizuri sana cha sheria ya dini. Mke wake alitoa ushuhuda kuwa, bwana Athmani alikuwa mume mwema, mwenye kuunganisha undugu, kumjali sana mama yake. Maisha yake yote yalikuwa mfano wa kufanya bidii katika shuguli zake pamoja na kuwalea vizuri watoto wake. Bwana Athmani alikuwa anawanasihi watoto wake kwamba , matendo yenu na dhati yenu yatoe ushuhuda juu ya uwepo wa Allah. Alikuwa anasema mujifaidishe na vipawa vyenu vyote kwa kuvitumia vizuri na kila amali yenu iwe kwa ajili ya kupata ridhaa ya Allah Mtukufu. Aliwafundisha watoto namna ya kuwapendelea wengine juu ya dhati yao yenyewe pamoja na unyenyekevu na kuhifadhi majina yote ya sifa ya Allah. Bwana Athmani alikuwa mtiifu sana kwa Khalifa na kujali zaidi nidhamu ya Jamaati. Alikuwa Mwema sana hata katika ujana wake na kufanya matendo mazuri kwa upendo na uaminifu. (rafiki yake Bwana Athmani. Watu walikuwa wanafaidika na maombi yake hata wale wasio wanajamaati. Alikuwa anazingatia sana sala zote na kusali kwa jamaa hata katika nyakati za kunyeshwa kwa mvua na kusali Tahajjudi kila siku. Alikuwa mhubiri mkubwa na kuwahubiri watu kwa jazba kubwa zaidi, naye alikuwa uhusiono huu kwa watu wengineo, wabashiri wetu wanasema popote tunapoenda tunawakuta watu kadhaa ambao humkumbuka bwana UTHMANI. Alikuwa mwenye kutoa rai nzuri na mushawara mwema kwa kila mtu.

Hadhrat Amir-ul-Muminiin alieleza matukio kadhaa juu ya kupokelewa kwa maombi yake na utawa wake na kumwombea dua kuwa Allah Amyanyue madaraja yake huko peponi na Kuwawezesha watoto wake kuwa warithi wa wema wake. Amin. Huzur alisema mara baada ya kumaliza Ijumaa nitasalisha sala yake ya jeneza InshaAllah.

Safari Ya Umrah Na Taratibu Zake

Na Ali R. Mohammed – Morogoro

Kwa Fadhila za Allah, tungependa kuzungumzia ibada ya Umrah au Hajji ndogo.

Hijja au Haji kama ilivyozoeleka ni moja Kati ya Mihimili au nguzo za dini ya Kiislam, ingawa katika nguzo hii ya 5, Mkazo upo kwa wale tu watakaoweza kufanya safari kuifikia KAABA, nyumba ya Mwenyezi Mungu huko Makkah. Ibada ya Hajji hufanyika katika mwezi wa Dhul Hijja tu, lakini Hija ndogo yaani Umrah inaweza kufanyika katika wakati wowote. Anayefanya Hajji ndogo hutekeleza karibu yote yanayofanywa katika Hijja kubwa isipokuwa kuchinja mnyama, na Ishara ya kumpiga Shetani katika eneo la Jamarat huko Mina Kaskazini mwa Masjid Haraam Makkah.

Aidha hujjaji wa Umrah huweza kuzuru maeneo yote matakatifu ya kihistoria na kupata nafasi ya kufanya maombi.

Ndugu yetu mmoja ambaye amepata nafasi ya kufanya Ibada hii ya Umrah katika miezi ya karibuni, anatuletea maelezo kuhusu yale ambayo tunaweza kujifunza kuhusu muhimili huu wa tano kati ya mihimili ya dini yetu ya islam.

1. **Maandalizi ya Ibada, Umrah au Haji**

Kama ilivyo ada, hujjaji wa Umrah hujiandaa kwa mahitaji muhimu kukamilisha safari hii ya Ibada.

Sehemu au kituo cha kwanza baada ya kuwasili nchini Saudia Arabia, ni katika mji mdogo wa MIQAAT.

Mahala hapa ni muhimu sana kwa Mahujaji wote wa Hijja kubwa na Ile ndogo ya Umrah, ambapo Maandalizi yote kabla ya kuingia mji mtakatifu wa Makkah hufanyika hapa.

Hujaj baada ya kuwasili Miqaat, huoga vizuri na kuchukua udhu kama ilivyo ada.. na huacha mavazi yake ya kawaida na kuvaa mavazi maalumu IHRAAM kwa ajili ya Ibada ya Hijja.

Hizi ni Shuka mbili nyeupe ambazo hazijashonwa. Neno la Kiarabu Ihraam maana yake Utukufu hivyo kuvua mavazi yetu ya kawaida na kuvaa Ihraam ni ***kuvua mateso yetu maovu na dhambi, na kuuvaa utakatifu wakati tunataka kuingia katika eneo tukufu la Mwenyezi Mungu***. Baada ya kuvaa vazi hili, hujjaji huingia katika msikiti uliopo hapo Miqaat na kusali rakaa 2 kujiweka tayari kimwili na kiroho,



ikiwa ni kuomba Allah kuwa wakati huo wewe ni mgeni Wake, na sasa unatarajia kuelekea katika nyumba Yake tukufu, ambayo ndiyo ya kale zaidi ya kuabudia na ni kitovu cha Ukuu na Umoja wa Mwenyezi Mungu.

Baada ya kukamilisha maandalizi ya usafi na kuvaa Ihram, mahujjaji kila mmoja kwa nafasi yake, anasali rakaa mbili za Sunna, na kufanya maombi tayari kwa safari kuelekea katika nyumba ya Allah.

SAFARI KUELEKEA MJI MTAKATIFU WA MAKKAH

Baada ya maandalizi yote, safari ya kuelekea Makkah huanza. Ni safari ya kilomita 9, ambayo huchukua takriban dakika 15 hivi.

Hapa ndipo huanza kushuhudiwa shani na utukufu wa Allah Muumba. Muda huu hujjaji hujihisi ni mwepesi kabisa, na pengine mwili si wake tena. Mapigo ya moyo hubadilika pia, hii ni kutokana na furaha, lakini yenye hofu pia juu ya Allah. Kwa kawaida Makkah ipo Bondeni. Hivyo unapotoka Miqaat huwa ni mteremko kiasi, hivyo hujjaji hujiona

Endelea uk. 9